JACKPOT BABA LAO!
TZS. 374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 2

**WANAOTUMIA** majina ya viongozi kukwepa kodi kikaangoni




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
Jumapili Oktoba 16, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581100
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## MTAALAMU KWA MKEMIA MKUU:

# MIDOLI INA SUMU

**NI** chanzo figo kuharibika, fizi kuwa za bluu... *Endelea ukurasa 4*





Rais Samia Suluhu Hassan akiomba dua kwenye kaburi la Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli nyumbani kwake Chato mkoani Geita jana. **Picha kulia:** Rais Samia akimsalimia Bibi Suzana Magufuli, ambaye ni mama mzazi wa Hayati Dk. Magufuli. **PICHA: IKULU**

# Samia avutiwa na Geita

UKURASA 2

UKURASA WA 2

### SHAKA: SAMIA NI PUMZI MPYA YA MAENDELEO

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka amesema kutokana na kasi ya kutekeleza miradi ya maendeleo nchini, Rais...

UKURASA WA 3

### DC ATOA ONYO WATOTO KUJILEA



MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Khadija Ali amekemea wazazi na walezi wasiosimamia malezi ya watoto....

UKURASA WA 3

### WAKURUGENZI LAWAMANI KWA KUTAFUNA FEDHA ZA WATUMISHI

WAKURUGENZI katika baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Singida wanadaiwa kutumia fedha za makato ya akiba ya Vyama vya Kuweka na Kukopa...

## Sungusungu wapewa kazi kuzuia ndoa wahitimu la 7

UKURASA 5

MICHEZO SIMBA, YANGA, AZAM KAZINI UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

# Samia avutiwa na Geita

**Na Daniel Limbe,** CHATO

RAIS Samia Suluhu Hassan amevutiwa na amani, utulivu na mazingira mazuri ya Mkoa wa Geita, akiahidi kuwa mkazi wa mkoa huo kwa muda usiojulikana.

Kauli hiyo aliitoa jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Chato muda mfupi baada ya kutembelea Hospitali ya Rufani ya Kanda Chato na baadaye Katoro wilayani Geita.

"Ninaomba nirudie kauli yangu niliyoitoa kule Chato baada ya kutembelea hospitali kubwa ya rufani ya kanda. Mimi ni mwana Geita na ninawaahidi nitakuja kuishi mkoani Geita muda fulani," alisema na kushangiliwa na umati wa wananchi.

Rais Samia aliwapongeza wananchi wilayani humo na wa Mkoa wa Geita kwa ujumla kwa kuendelea kuchapa kazi na kuwasisitizia kuongeza kilimo cha mpunga na mazao mengine ili kujikwamua kiuchumi.

Pia aliwapongeza wabunge wa Mkoa wa Geita kwa kuwasilisha kwake mahitaji ya wananchi ambayo serikali inaendelea kuyatatua ikiwamo ujenzi wa barabara za lami na za mitaa na uwekaji wa taa barabarani.

Rais Samia aliwasili jana wilayani humo kwa ziara ya kikazi, akitoka Kagera kwenye sherehe za kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru zilizoambatana na kumbukizi ya miaka 23 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Akiwa wilayani Chato, Rais Samia alitembelea kaburi la Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli nyumbani kwake Rubambangwe Mlimani kisha kumsalimia mama mzazi wa Dk. Magufuli, Suzan Joseph kabla ya kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda Chato.

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa Chato Kati, Hamis Mwitazi alimpongeza Rais Samia kwa kufanya ziara hiyo ambayo inafufua matumaini ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na Hayati Dk. Magufuli.

Mbunge wa Chato, Dk. Medard Kalemani alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia kwa jitihada kubwa za kuiongoza nchi na kudumisha amani na mshikamano.



Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Alhaj Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akitembezwa katika maktaba kwenye jengo la ukumbi mpya wa mikutano wa Msikiti Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wa Mohamed wa Sita, Kinondoni Muslim, mkoani Dar es Salaam, baada ya kuhudhuria Swala ya Ijumaa, juzi. **PICHA: MUHIDIN MICHUZI.**

# Shaka: Samia ni pumzi mpya ya maendeleo

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka amesema kutokana na kasi ya kutekeleza miradi ya maendeleo nchini, Rais Samia Suluhu Hassan ni 'pumzi mpya kwa maendeleo ya nchi'.

Shaka alitoa kauli hiyo jana alipowasilisha salamu za chama hicho wakati wa mkutano wa hadhara uliohutubiwa na Rais Samia wakati wa ziara yake mkoani Geita.

Alitumia fursa hiyo kukumbusha kuwa tangu Rais Samia alipoingia madarakani Machi 19 mwaka jana, mambo makubwa yamefanyika.

"Sisi ambao tumekuwa na wewe leo tangu asubuhi ni mashahidi, tumekwenda pale katika Hospitali ya Kanda ya Chato. Hospitali ile ni ukombozi mkubwa kwa wananchi kwa kuwa itatibu hata magonjwa sugu," alisema.

Shaka alisema mbali na Hospitali ya Kanda ya Chato, katika eneo la Kanda ya Ziwa, pia kuna hospitali kubwa ikiwamo ya Kanda Bugando ambayo inashirikiana na Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) kutoa matibabu ya saratani na Hospitali ya Nyerere iliyoko Musoma mkoani Mara inayoshirikiana na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) kutibu maradhi ya mifupa.

Mbali na sekta ya afya, Shaka alisema Rais Samia ameendelea kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa na chama kwa ajili ya kuleta maendeleo.

"Sasa ni wakati wa kwenda bega kwa bega na Rais Samia kuleta maendeleo. Rais Samia ni pumzi mpya ya maendeleo kwa nchi yetu," alisifu.

Shaka alitumia fursa hiyo kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia katika kuleta maendeleo kwa kuwa tangu ameingia madarakani, hakuna kilichosimama.

Kiongozi huyo wa CCM pia alitoa hadhari na kuonya kuhusu rushwa katika kusimamia miradi ya maendeleo, akisisitiza kuwa chama chao kitaendelea kuwa karibu katika utekelezaji wa miradi hiyo.

## Wanaotumia majina ya viongozi kukwepa kodi nchini kukiona

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameiagiza Mamlaka ya Mapato (TRA) kuwafuatilia wafanyabiashara wanaotumia vibaya majina ya viongozi wakiwamo wa kitaifa, kukwepa kodi ya serikali.

Majaliwa alitoa angalizo hilo jana akiwa kwenye ziara ya kukagua upanuzi wa mashamba ya miwa na mitambo iliyoongezwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera Sugar kilichoko Misenyi mkoani Kagera.

Kiwanda hicho kimeongeza uzalishaji wake kutoka tani 60,000 na kufikia tani 110,000 kwa mwaka.

Akizungumza katika ziara hiyo, Majaliwa alisema kila anayefanya biashara, hata kama ni kiongozi, anapaswa kulipa kodi.

"TRA endeleeni kuchukua hatua hata kwa kumfuata kiongozi aliyetajwa ili mjiridhishe kama kinachosemwa na mfanyabiashara ni sahihi. Kwa kuwa matumizi mabaya ya majina ya viongozi yanawasumbua sana watumishi wa TRA," aliagiza.

Vilevile, kiongozi huyo aliiagiza TRA kuendelea kusimamia kikamilifu sheria za ukusanyaji wa mapato kwa kuwa yeyote aliyeamua kufanya biashara nchini, anapaswa kuhakikisha ulipaji kodi unapewa kipaumbele.

Majaliwa pia aliitaka TRA ichukue hatua dhidi ya mfanyabiashara atakayebainika kukwepa kodi.

Kuhusu kiwanda hicho, Majaliwa alisema maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya nchi kujitosheleza kwa uzalishaji wa sukari, yanafanyiwa kazi baada ya kiwanda hicho kuongeza uzalishaji.

Alisema kitendo cha kiwanda hicho kuendelea kuweka mikakati ya kuboresha na kukuza uwekezaji, kitaongeza kiwango cha uzalishaji wa sukari na kuipungua serikali gharama ya uagizaji bidhaa hiyo nje ya nchi. Pia alisema kiwanda hicho ni fursa kwa wakazi wanaoishi katika vijiji jirani ambao wanajiajiri kupitia kilimo cha miwa na kuwa na uhakika wa soko.

"Uwekezaji wenu utawezesha kuongeza kiwango cha uzalishaji wa sukari nchini. Hii itawezesha nchi kupunguza kiwango cha sukari tunachoagiza kutoka nje.

"Mkakati wenu wa upanuzi wa kiwanda uende sambamba na ushirikishwaji wa wananchi waishio katika vijiji vinavyowazunguka ili nao waongeze mashamba ya miwa," aliagiza.

Majaliwa alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Misenyi, Kanali Wilson Sakulo kuweka mkakati wa kuhamasisha wananchi wa vijiji 13 vinavyozunguka kiwanda hicho, kulima miwa kwa wingi ili kujiongezea kipato na kuongeza idadi ya malighafi inayohitajika kiwandani huko.

"Viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), tutaendelea kumsaidia Rais Samia kuhakikisha yote yaliyoahidiwa yanatekelezwa," aliagiza.

Aliwahakikishia wawekezaji hao kuwa serikali itaendelea kuwapa ushirikiano ili malengo waliyoyaweka katika uwekezaji huo, yafikiwe na kuongeza tija kwao na taifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kiwanda cha Kagera Sugar, Seif Ali Seif alisema wameongeza uzalishaji, wakiwa na matarajio ya kuzalisha tani 110,000 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Miaka mitano iliyopita walikuwa wanazalisha tani 60,000 kwa mwaka.

"Lengo letu ni kuzalisha tani 300,000, kwa sasa tumeajiri watumishi 10,000, tunaishukuru serikali kwa ujenzi wa Daraja la Kitengule ambalo linasaidia kusafirisha malighafi za kiwanda kwa urahisi," alisema.

HABARI KITAIFA

# Newala yaanza kutekeleza maagizo upimaji maeneo

**Na Mwandishi Wetu,** NEWALA

HALMASHAURI ya Mji wa Newala mkoani Mtwara imeanza kutekeleza maagizo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula ya kuzitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha zinapima na kumilikishwa maeneo yake yakiwamo ya shule, zahanati na vituo vya mabasi ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Newala, Shamim Mwariko jana alikabidhiwa jumla ya hati saba na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mtwara, Rehema Mwinuka ambapo hati tano kati ya alizokabidhiwa ni za shule za msingi na mbili za zahanati.

Shule za msingi zilizopata hatimiliki za ardhi ni Mtangalanga, Kiduni, Butiama, Mcholi II na Mkoma I huku zahanati zikiwa ni Mkoma I na Makondeko.

Akizungumza baada ya kukabidhi hati hizo mkoani Mtwara jana, Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Mtwara, Rehema Mwinuka, aliipongeza Halmashauri ya Mji wa Newala kwa uamuzi wa kupimiwa maeneo yake na kuzitaka halmashauri zingine katika mkoa huo kuiga mfano wa halmashauri hiyo kwa kupima na kumilikishwa maeneo yake ili kuepuka uvamizi katika maeneo hayo.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza Halmashauri ya Mji wa Newala kwa uamuzi wenu wa kupima maeneo yenu, hii itasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi inayotokana na uvamizi na niombe halmashauri nyingine ziige mfano wenu," alisema Rehema.

Mbali na kukabidhi hati kwa Halmahauri ya Mji wa Newala, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mtwara aliwaongoza watumishi wa mkoa wake kutoa hati kwa wamiliki wa ardhi waliokamikisha taratibu za kupatiwa hati sambamba na kusikiliza na kutatua kero za sekta ya ardhi katila kituo jumuishi.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanzisha utaratibu wa ofisi zake za ardhi katika mikoa kuwa na vituo jumuishi vya kusikiliza na kutatua kero za ardhi pamoja na kutoa hatimiliki za ardhi ikiwa ni juhudi za kusogeza huduma karibu na wananchi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi maalum wa maeneo ya wazi nchini ya Machi 2017, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alibainisha kuwa maeneo ya wazi mengi yamevamiwa na kuitaka serikali kuchukua hatua.



Dereva wa boda-boda akiwa ameshe-heni mzigo wa mkaa na kumfanya ashindwe kuona nyuma, eneo la Mwanambaya, wilayani Mkuranga mkoani Pwani mwishoni mwa wiki, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wakurugenzi lawamani kwa kutafuna fedha za watumishi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKURUGENZI katika baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Singida wanadaiwa kutumia fedha za makato ya akiba ya Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) ambayo ni michango ya hiari waliyojiwekea watumishi wa vyama hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akifunga mkutano wa Jukwaa la Maendeleo ya Vyama vya Ushirika Mkoa wa Singida jana, alisema hali hiyo imesababisha SACCOS za watumishi kukosa fedha za kukopesha wanachama na hivyo kuingia kwenye migogoro isiyo ya lazima.

"Niwaelekeze wakurugenzi wote ambao wanadaiwa na SACCOS za watumishi kulipa fedha hizo mara moja ili watumishi waweze kupata mikopo," alisema.

Serukamba aliwagiza viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika kusimamia na kuendesha vyama hivyo kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na kujiepusha na ubadhirifu unaosababisha vizorote.

Alisema serikali haitawavumilia viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika watakaofanya ubadhirifu na kusababisha hasara katika vyama hivyo na yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aliongeza kuwa wakurugenzi wa halmashauri kwa kushirikiana na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Singida kuweka mpango katika kila halmashauri kuanzisha vyama vya ushirika hususani vya mazao ya kimkakati kama vile korosho, mkonge, tumbaku na alizeti.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Singida, Nipaneema Mfuru, alisema shida iliyopo ni wakurugenzi kushindwa kuwasilisha makato yaliyokatwa kutoka hazina kupitia kwenye akaunti za halmashauri kwa zaidi ya miaka sita kwa SACCOS za watumishi.

Alisema shida nyingine ni maofisa ushirika kuendelea kuwa katika mamlaka mbili za kiutawala na hivyo kusababisha baadhi yao kupangiwa kazi tofauti na majukumu hayo na utendaji kazi kupungua.

Mfuru alisema ofisi ya Mrajis Msaidizi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ina mkakati wa kutoa elimu ya udhibiti na kupamba na rushwa katika vyama vya ushirika.

Mkakati mwingine ni kuendelea kuimarisha Vyama vya Ushirika 'sinzia' ambavyo vipo 278 na kutoa elimu na kuanzisha vingine vitakavyojibu mahitaji ya wananchi wa Mkoa wa Singida.

Mkoa wa Singida hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu ulikuwa na jumla ya Vyama vya Ushirika 373 lakini ambavyo vipo hai ni 95 tu.

## DC atoa onyo watoto kujilea

**Na Sabato Kasika,** aliyekuwa Mkuranga

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Khadija Ali amekemea wazazi na walezi wasiosimamia malezi ya watoto wao wilayani humo, akionya kuwa serikali itawachukulia hatua za kisheria dhidi yao bila huruma.

Alitoa onyo hilo juzi wilayani humo wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Mafunzo ya Ufundi cha Reach the Goal kwa ajili ya mabinti waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Kituo hicho kinachosimamiwa na shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization (HDO) kwa ushirikiano na Shirika la Lutogo Development Initiative, kiko eneo la Mwanambaya wilayani Mkuranga.

Mkuu wa wilaya huyo alisema baadhi ya wazazi wameacha wajibu wao wa kulea watoto na kuwafanya wajilee, hali ambayo inasababisha waingie katika vishawishi vinavyochangia washindwe kuendelea na masomo.

"Ninawatangazia wazazi na walezi wote ambao hamtimizi wajibu wenu wa malezi, serikali itawachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwakamata na kuwafikisha mahakamani kama hamtasimamia malezi," alionya Khadija.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiilaumu serikali, hata pale watoto wao wanapofanya maovu katika jamii wakidai imeshindwa kudhibiti vitendo viovu bila kutambua kuwa chanzo cha tatizo ni malezi duni.

"Mkuranga ina matukio mengi ya aina mbalimbali yakiwamo ya ndoa utotoni, mabinti kupewa mimba huku wazazi wakimalizana na wahalifu kwa kuwa ni ndugu zao, wanafichia siri au wanawapoza kwa fedha," alisema.

Khadija alisema hataki kuona hayo yakiendelea wilayani mwake na kwamba kila mzazi na mlezi atimize wajibu wake katika malezi na kuwa tayari kutoa taarifa kwa vyombo vya dola pale wanapoona kuna viashiria vya ukatili kwa watoto.

"Kumbukeni kwamba mzazi au mlezi kumwozesha mtoto ni kumfanyia ukatili na kumkatisha masomo na kumfanya asitimize ndoto zao.

"Hivyo, niwaombe wanawake kuwa mstari wa mbele kukemea na kutoa taarifa ya matendo yote maovu dhidi ya watoto wote wakiwamo wa kiume," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Himiza, Prisca Ngweshemi alisema kituo kimeshapokea mabinti 70 ambao wataanza mafunzo ya ufundi mbalimbali ikiwamo kushona nguo kutengeneza batiki na taulo za kike.

"Tumejikita katika harakati za kupambana na ukatili wa kijinsia kwa vijana wa kike kwani umeendelea kuwa tatizo kubwa na tishio kwa jamii yetu, tunataka watimize ndoto za kupitia ujuzi watakaoupata," alisema Prisca.

Alifafanua kuwa maafunzo yataanza rasmi mwishoni mwa mwezi huu, yakiendeshwa na shirika lake kwa ushirikiano na shirika lingine la Lutogo Development Initiative pamoja na wadau wa kutetea haki za mtoto wa kike.

Alisema katika harakati zao za kuelimisha jamii kuachana na mtindo wa kukwamishwa mabinti, kuna vikwazo wanakumbana navyo kutoka kwa baadhi ya wazazi wanaokumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati.

"Lakini pia wapo baadhi ya wazazi wanadai wana hali duni ya maisha ambayo inawafanya wawakatishe masomo mabinti zao ili waolewe, wapate mahari. Hayo yote na mengine ni hatari kwa ustawi wa mtoto wa kike," alisema.

Mwanzilishi wa Lutogo Development Initietive, Lulu Mwalubandu alisema shirika lake limeamua kuungana na Himiza kwa hali na mali ili kuwakomboa watoto wa kike wilayani Mkuranga.

# Mtaalamu afichua midoli ina sumu

## •Ni chanzo figo kuharibika, fizi kuwa za buluu



**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

OKTOBA 23 hadi 27 kila mwaka, dunia huadhimisha wiki ya kuzuia sumu ya madini ya risasi. Nchini madhara makubwa yametajwa kuwapata watoto kupitia midoli ya kuchezea na rangi za ukutani.

Mratibu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Yohana Goshashy, katika mazungumzo mahsusi na Nipashe jana, alieleza kwa kina ukubwa wa tatizo hilo nchini.

Anasema watoto wanapata sumu hiyo kwa kucheza katika maeneo yenye rangi inayobanduka kwa sababu wanaweza kuibandua kwa mikono na kuiweka mdomoni.

"Wakishika wanatakiwa kunawa kwa maji na sabuni kabla ya kula chakula ili kuepuka madhara," Goshashy anashauri na kubainisha kuwa midoli ya kuchezea watoto ina sumu ya madini ya risasi, hivyo bila kufahamu watoto hupata madhara.

Anasema kuwa ili kuepuka tatizo hilo, kunatakiwa kuwapo sheria na sera za kuzuia matumizi ya rangi au midoli ya watoto yenye madini ya risasi.

"Pawe na alama ya kuonyesha rangi zisizo na madini ya risasi katika vifungashio," Goshashy anasisitiza.

**CHANZO CHA SUMU**

Madini ya risasi hupatikana kwenye gamba la uso wa dunia; kwa watengenezaji wa betri za magari na redio; kwa wahunzi; watengenezaji wa glasi; rangi za kuta hususani zinazoondolewa.

Goshashy anasema vyanzo vingine vya sumu ya risasi ni pamoja na rangi ya kuchimba au rangi ya kale ya risasi katika nyumba ambazo zilijengwa kabla ya rangi ya risasi kupigwa marufuku mwaka wa 1978 kwa baadhi ya nchi.

Gushashy anataja chanzo kingine cha kawaida cha risasi ni maji ya kunywa, ikiwa yanatolewa kupitia mabomba ya zamani ya risasi.

"Kwa sababu risasi haiharibiki baada ya muda, udongo katika yadi au kando ya barabara unaweza kuwa na risasi, tangu siku ambazo petroli ilikuwa na madini ya risasi au kama matokeo ya vipande vya rangi ya risasi kutoka maeneo ya zamani ya viwanda na nyumba," anafafanua.

Anasema kuwa kutokana na madhara ya sumu ya madini ya risasi, Shirika la Afya Duniani (WHO) limeziunganisha nchi kufanya madhimisho ya kuzuia sumu ya madini ya risasi duniani kwa kutenga wiki ya Oktoba 23 hadi 26 ya kila mwaka kujenga uelewa wa kuzuia matukio ya sumu ya madini ya risasi.

Goshashy anasema kaulimbiu kwa mwaka huu ni 'Sema hapana kwa matukio ya sumu ya madini ya risasi', akisisitiza kuwa Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu kinaunga mkono kaulimbiu hiyo kwa kutoa elimu ya kujikinga kupitia vyombo vya habari.



Yohana Goshashy

**DALILI ZA SUMU**

Goshasy anasema kwa kawaida sumu ya madini ya risasi hurundikana mwilini na hukaa kwa muda wa miezi au miaka kadhaa na haina faida yoyote kwenye mwili wa binadamu.

Anasema sumu hiyo inaweza kuathiri ubongo na viungo vingine muhimu na kusababisha mabadiliko ya mishipa ya fahamu (neva) na tabia, ugonjwa wa utumbo, kuharibika kwa figo na ucheleweshaji wa ukuaji hususani kwa watoto.

Alisema dalili za sumu hiyo mara nyingi huwa hafifu na ni ngumu kuzigundua kwa sababu zinafanana na za magonjwa mengine.

Goshashy anataja dalili hizo kuwa ni kuwashwa au hisia za ganzi (neuropathy), uchovu, kuumwa na kichwa, kupoteza umakini, upungufu katika kumbukumbu ya muda mfupi, kizunguzungu na kupoteza uratibu wa mwili.

Anataja dalili zingine kuwa ni kukosa uwezo wa utambuzi wa ladha mdomoni na fizi kupata mstari wa bluu, hali inayojulikana kama mstari wa Burton.

Anasema mwenye dalili hupata maumivu ya tumbo, kichefuchefu na kutapika, kuhara au kuvimbiwa na watoto wadogo hupata mabadiliko makubwa ikiwamo kushindwa kufanya vizuri darasani, tofauti na watoto wasio na tatizo hilo.

Goshashy anasema wakati mwingine mtu hupata ulemavu wa kudumu wa kiakili, kupata shinikizo la damu, kutosikia, mtoto wa jicho, utasa kwa wanaume, kuharibika kwa mimba na watoto kuzaliwa kabla ya wakati.

**MBINU KUBAINI TATIZO**

Goshashy anasema sumu ya risasi inaweza kutambuliwa kupitia aina mbalimbali za vipimo vya maabara za afya na kiuchunguzi ikiwamo Maabara ya Uchunguzi Sumu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na mashine za X-Ray.

Anasema vipimo hivyo ni vile vya mkusanyiko wa risasi kwenye damu ambavyo hutumia (➔g) kwa kila desilita (dL) ya damu.

**MATIBABU YAKE**

Goshashy anasema njia kuu ya matibabu ya sumu itokanayo na madini ya risasi ni tiba inayoitwa kwa kitaalamu 'Chelation'.

Anasema tiba hiyo inahusisha matumizi ya mawakala wa 'chelating' ambayo hufunga kikamilifu chuma na kuunda kiwanja kisicho na sumu ambacho kinaweza kutolewa kwa njia ya mkojo kwa urahisi.

"Mfano wa wakala wa Chelation ni EDTA (asidi ya ethylene diamine tetra-asetiki)," anatoa ufafanuzi wa kitaalamu.

**KUZUIA SUMU**

Goshashy anasema wananchi wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kujua afya zao na kuwa na taarifa kama walishawahi kuwa katika mazingira ya sumu hiyo.

Anasema kama watu wanaamini walipita katika maeneo hayo, wanatakiwa kutoa taarifa katika Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti matukio hayo.

Anasema jamii pia inatakiwa kuhakikisha familia inakula vyakula vya viwango vya juu vya madini ya Calcium, chuma na Vitamini C.

"Virutubisho hivi husaidia kupunguza viwango vya risasi katika damu na hivyo vinaweza kupunguza hatari ya sumu ya risasi," anafafanua.

Goshashy anasema jamii inatakiwa kuepuka kuwa na matumizi ya mabomba ya risasi katika maeneo inakoishi au kufanya kazi.

Pia anasema waliokutana na tatizo hilo, wanatakiwa kuzingatia matibabu ya haraka ili kuepuka kupata madhara zaidi.

Anatoa rai kwa jamii kubadili tabia ya kutokuchua tahadhari ya kuepuka sumu ya risasi.

**USULI**

Madini ya risasi yamekuwa na madhara kwa miaka mingi na jitihada za kuyapunguza zilianzishwa na mashirika mbalimbali ya kimataifa.

Mkataba wa kimataifa wa kudhibiti matumizi ya risasi nyeupe uliidhinishwa katika Kongamano Kuu la Shirika la Kimataifa la Kazi (ILO) tangu mwaka 1921 na kuridhiwa na mataifa 63.

Goshashy anawataka wananchi kutoa taarifa wanapokutana na matukio ya sumu za madini ya risasi kwa kupiga simu bure namba 022 2221410 na 0736 613333 ili kupata msaada wa haraka.

## Wabunge wataka elimu ya Ebola kwa wananchi

**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

WAJUMBE wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii wamesema elimu inahitajika zaidi katika kuendelea kudhibiti ugonjwa wa Ebola kuingia nchini.

Pia wamepongeza juhudi zinazofanywa na Wizara ya Afya kutoa elimu mipakani na kuweka wataalamu wa afya kwa ajili ya kuwapima wageni wanaoingia nchini kutoka nchi jirani.

Mbunge wa Nanyamba mkoani Mtwara, Abdallah Chikota alitoa rai hiyo juzi wilayani Bukoba mkoani Kagera alipozungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kuhitimishwa kwa kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru.

"Ninaunga na Rais Samia Suluhu Hassan (aliyehitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru) kuwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya. Wizara ya Afya nayo iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu hatari ya ugonjwa huu ili waendelee kujikinga," alisema.

Chilota alisema kazi kubwa ya kamati yao ni kuendelea kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari zote na wananchi kuzingatia kanuni za afya ili kudhibiti ugonjwa huo, hasa kwa kuzingatia Mkoa wa Kagera upo jirani na Uganda ambako ugonjwa huo umerpotiwa kulipuka.

"Kazi yetu kama wabunge, tuna wajibu wa kuendelea kufanya kampeni ya kuelimisha jamii ili usiingie nchini na juhudi hizi zitasaidia kama ambavyo ugonjwa wa UVIKO-19 ulivyoingia nchini na kudhibitiwa," alisema Chikota.

Mbunge wa Buyungu mkoani Kigoma na mjumbe wa kamati hiyo, Aloyce Kamamba aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zinazotolewa na wizara hiyo.

Pia aliitaka wizara kuendelea kuwekeza nguvu ya kutoa elimu katika mikoa yote nchini kwa kuwa nchi zina mipaka lakini ugonjwa hauna mipaka.

"Ninatambua juhudi kubwa zilizofanywa na Wizara ya Afya, ninaomba tuendelee sasa kuhimiza elimu iendelee kutolewa maeneo yote nchini, jamii ichukue tahadhari zote zinazotakiwa katika kujikinga na maambukizi kama taifa," alisema Kamamba.

Kaimu Mkurugenzi wa Kinga, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Wizara ya Afya, Dk. Amma Kasangala alisema wametumia sherehe za kuhitimisha mbio za Mwenge kufikia kundi kubwa la wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi.

Alisema kupitia elimu waliyotoa, wanaamini jamii itaendelea kuchukua tahadhari zote na kuhakikisha ugonjwa huo hauingii nchini.

Alisema tangu kuingia kwa ugonjwa huo, wamefanikiwa kutoa elimu katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo mikoa iliyoko mipakani hususani Mkoa wa Kagera.

# Wizara yaonya wadau hujuma dhidi ya NHIF

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel ametoa angalizo kwa wadau wa sekta ya afya kuepuka ubadhirifu ili kuulinda Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Amesema vitendo vya ubadhirifu kwa watumishi wa sekta ya afya vimekuwa vikitajwa mara kwa mara katika sekta ya afya, hivyo visipodhibitiwa vitauua mfuko huo.

Dk. Mollel alitoa kauli hiyo jana, akisisitiza kuwa sekta ya afya imetajwa kuwa ni ya pili kwa kukithiri vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma, hivyo suala hilo lisipojadiliwa kwa undani litakwamisha na kurudisha nyuma utoaji huduma katika sekta ya afya.

Kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Dk. Mollel alisema itakapoanza kufanya kazi, italeta faida lukuki, mojawapo ikiwa ongezeko la ajira.

"Ajira zitaongezeka, watu watafungua huduma za afya sehemu mbalimbali ikiwamo vijijini kwa sababu watakuwa na uhakika wa kupokea wananchi wengi wenye bima za afya," alisema Dk. Mollel.

**CHANJO CORONA**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi alisema hadi sasa asilimia 70 ya Watanzania wameshapata chanjo ya ugonjwa wa corona.

Kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa Ebola, Prof. Makubi alisema serikali inachukua hatua ya kuudhibiti ili usiingie nchini.

Alisema serikali imeweka uangalizi mkubwa katika mikoa ya Kigoma, Mwanza, Arusha na Kagera kuhakikisha ugonjwa wa Ebola hauingii nchini.

Kuhusu utoaji huduma bora za afya, Prof. Makubi alivitaka vyuo vikuu na vyuo vya kati kutoa huduma bora za afya, akisisitiza kuwa wadau wote wa sekta ya afya wanapaswa kuhakikisha kunakuwa na huduma bora za afya kuliko kuzi-achia hospitali.

Prof. Makubi alisema bima ya afya kwa wote itakapoanza kufanya kazi, itakuwa ni mkombozi kwa Watanzania wengi hususani wanaoishi katika umaskini.

Alisema Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote itakapoanza kufanya kazi, serikali inatarajia asilimia 85 ya Watanzania watajiunga katika kupata huduma hiyo.



Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (katikati), akijadiliana jambo na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022, Sahili Nyanzabara Geraruma, wakati wa maadhimisho ya kilele cha mbio za Mwenge huo, katika Uwanja wa Kaitaba, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sungusungu wapewa jukumu kuzuia ndoa wahitimu la VII

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Jadi (Sungusungu) Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Shinyanga limepewa jukumu la kuhakikisha hakuna ndoa ya utotoni ya mwanafunzi yeyote aliyehitimu darasa la saba mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko aliwakabidhi jukumu hilo juzi wakati wa kusimikwa viongozi wapya sita wa Jeshi la Jadi (Sungusungu) Tarafa ya Shinyanga Mjini.

Alisema wanafunzi waliohitimu darasa la saba wako majumbani wakisubiri matokeo ya kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, hivyo hataki kusikia wanafunzi hao wakiozeshwa ndoa za utotoni huku akilitaka jeshi hilo liwe mlinzi wa watoto hao.

"Sitaki kusikia mtoto ameozeshwa na ninyi Jeshi la Jadi mpo, zuieni ndoa hizi ili matokeo yakitoka ya kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, wakutwe wako salama na kuendelea na safari ya kutimiza ndoto zao kielimu.

"Fanye uchunguzi wa ndoa hizo na kuzidhibiti watoto hawa ni wetu sote lazima tuwalinde, ninawaomba na viongozi wa dini kemeeni matukio ya namna hii ya watoto kufanyiwa ukatili kwa kuozeshwa ndoa za utotoni, kunajisiwa na wakiume kulawitiwa ili jamii iwe salama," aliagiza.

Mkuu wa Wilaya huyo pia alilitaka jeshi hilo kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama katika mitaa yote pamoja na kudhibiti wimbi la vibaka mitaani ambao wamekuwa wakipora vitu mbalimbali zikiwamo simu na pochi za kinamama.

Ofisa Uhusiano na Umma kutoka Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Nsianel Gerald aliliomba Jeshi la Jadi kukomesha vitendo vya uharibifu wa miundombinu ya maji ambavyo kwa sasa vimekithiri na kusababisha ukosefu wa huduma ya maji kwa wananchi.

Mwenyekiti Mpya wa Jeshi la Jadi Sungusungu Tarafa ya Shinyanga Mjini, Paulo Madale aliahidi jeshi hilo litafanya kazi zake kwa weledi kukomesha vitendo vya uhalifu mitaani.

Alisema kuwa fedha ambazo watakuwa wakitoza za faini kutokana nma makosa mbalimbali, zitakuwa zikipelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Viongozi wapya wa Jeshi la Jadi (Sungusungu) Tarafa ya Shinyanga Mjini waliosimikwa ni Paul Madale (Mwenyekiti), Makamu wake, Juma Mipawa, Katibu Mkuu Ngaja Ngasa, Msaidizi wake, Lucas Shija, Kamanda Mkuu Thomas Mwita na Msaidizi wake Rashidi Ngoeji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Waliohusika madudu ya taarifa za Mwenge wawajibishwe wote*

**MWENGE** wa Uhuru ulihitimisha mbio zake juzi mkoani Kagera baada ya kukimbizwa katika wilaya zote za Tanzania na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo ulikopita.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa wakati wa kilele cha mbio hizo katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, mwenge huo ulikimbizwa umbali wa takriban kilomita 39,274 kuanzia Aprili 2, mwaka huu, katika Mikoa 31 na halmashauri 195 ndani ya siku 195. Katika mbio hizo, mwen ge huo ulizindua na kuweka mawe ya misingi katika miradi 1,293 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 650.

Licha ya kuzindua miradi hiyo, miradi 65 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 12.8 katika halmashauri 43 ilitiliwa shaka kutokana na kutekelezwa katika viwango duni au miradi hiyo ikiwa haina thamani inayoendana na fedha zilizotumika.

Kutokana na hali hiyo, kila sehemu ambayo miradi ilionekana kuwa na kasoro, kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa mwaka huu, Sahili Nyanzabara Geraruma, alikuwa akiweka wazi kwamba miradi hiyo haiwezi kuzinduliwa au kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Mbali na madudu hayo kwenye miradi, kiongozi huyo alisema Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unashindwa kuwafikia kimikopo walengwa kutokana na ubadhirifu katika baadhi ya halmashauri. Pia alisema katika baadhi ya maeneo, ilibainika kuwa asilimia kubwa ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya vijana, zimekuwa zikibanwa na zingine kubadilishiwa matumizi pamoja na kutokusimamiwa vyema.

Kutokana na kuibuliwa kwa madudu hayo, Rais Samia Suluhu Hassan, katika kilele cha mbio hizo za mwenge zilizoambatana na Kumbukumbu ya miaka 23 ya Kifo cha Mwalimu Julius Nyerere, aliagiza TAKUKURU na Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kuchunguza miradi iliyobainika kuwa na dosari.

Licha ya kuziagiza taasisi hizo, alizitaka kujichunguza kwanza kabla ya kutekeleza kazi hiyo kutokana na tabia ya kusubiri taarifa za wadhibiti na wakaguzi wakuu wa hesabu za serikali na ripoti za mbio za mwenge ndipo wazifanyie kazi badala ya kufuatilia wakati wa utekelezaji.


Taarifa za ubadhirifu ambazo zimekuwa zikiibuliwa katika ukaguzi mbalimbali zimekuwa sasa kama donda ndugu kutokana na kujirudia mara kwa mara licha ya maagizo kutoka ngazi za juu serikalini. Ni wakati mwafaka sasa ikatafutwa dawa ili kukomesha tatizo hilo ambalo linasababisha miradi ya maendeleo kufanywa kwa kiwango duni au kutokukamilika.

Kama alivyoagiza Rais, ni vyema TAKUKURU na ZAECA zikafanya uchunguzi wa madudu yaliyotokana na ripoti ya mwenge na wahusika kuchukuliwa hatua. Taarifa za uchunguzi zifanywe ndani ya muda mfupi ili serikali iwawajibishe viongozi na waliopewa jukumu la kutekeleza miradi hiyo.

Lakini pia kama alivyosema Rais, taasisi zilizopewa kazi ya kuchunguza na kufuatilia mienendo ya kuwapo kwa vitendo vya rushwa, zinapaswa kujitafakari kutokana na kuendelea kutamalaki kwa madudu kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo hugharimu mabilioni ya shilingi. Haiwezekani kila mwaka kujirudia taarifa zile zile wakati taasisi zenye dhamana hiyo zipo na zinaona ni jambo la kawaida.

Kwa maeneo ambayo miradi imebainika kuwa na matatizo na taarifa za uchunguzi zikaweka bayana, ni vyema wahusika wote, kuanzia maofisa waliopewa kazi ya kusimamia, makandarasi, wakurugenzi, wakuu wa wilaya na mikoa, wakawajibishwa bila kuonewa huruma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Viwanda vya kuchakata matunda ni mkombozi

**WIZARA** ya Kilimo imepewa jukumu la kusimamia kilimo cha maparachichi na kuwatafutia wakulima mbegu bora, kutunza miche shambani na kutafuta masoko, ili kunufaika na kilimo cha matunda hayo.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha wakulima wa matunda hayo wananufaika na kilimo chake ambacho kinatekelezwa kwenye baadhi ya mikoa ikiwamo ya Njombe, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro.

Ninakubaliana na mikakati hiyo yenye lengo la kumnyanyua mkulima wa matunda, kutokana na kwamba baadhi yao wamekuwa hawafaidiki na kilimo hicho kutokana na ukosefu wa soko la uhakika.

Hali hiyo inasababisha baadhi ya matunda kama machungwa kuoza kutokana na ukosefu wa soko na hivyo wakulima kujikuta wakipata hasara, hivyo kuwapo kwa soko la uhakika kunaweza kuwa mkombozi kwao.

Uhakika wa soko utasaidia kuwafanya wasiendelee kukusanya matunda na kumwaga chini kusubiri wateja bila kuwa na uhakika kama watawapata, badala yake watavuna na kwenda kuuza kule ambako tayari kuna soko la uhakika.

Ninakumbuka Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwahi kuwaagiza maofisa kilimo kuanzia wa mkoa hadi wilaya kuhakikisha wanawasaidia wakulima kulima kisasa zao hilo, huku wakurugenzi wakitakiwa kuwaondoa maofisa kilimo halmashauri wakafanye kazi kwa wakulima na kuanzisha mashamba darasa ya kufundishia wakulima.

Kimsingi, hatua hiyo yenye lengo la kuwasaidia wakulima wa matunda hayo, ni nzuri kwani kuwatafutia soko la uhakika, na wao watakuwa na uhakika wa sehemu ya kuuza matunda yao.

Hatua hiyo inaweza kuwasaidia waondokane na hasara za mara kwa mara ambazo wamekuwa wakikumbana nazo, ambazo zinasababishwa na ukosefu wa soko la uhakika na kuwafanya wajipatie fedha, kwa ajili ya maendeleo yao.

Lakini pamoja na hayo, ninadhani vingejengwa viwanda vidogo vingi vya kuchakata matunda nchini, hasa kwenye maeneo ambayo matunda yanapatikana kwa wingi, ili wakulima na sehemu ya uhakika ya kuyapeleka.

Kuwapo kwa viwanda vya kuchakata matunda kunaweza kuongeza soko la ndani, kuanzia maparachichi, machungwa, mananasi na matunda mengine, ambayo yamekuwa yakioza mashambani kutokana na ukosefu wa soko.

Viwanda hivyo pia vinaweza kusaidia juhudi za serikali za kutaka Tanzania kuingia katika masoko ya kimataifa, kwa kuuza bidhaa zinazotokana na matunda mbalimbali yanayopatikana nchini. Lengo la serikali ni kufikia Tanzania ya viwanda, hivyo nchi ikiwa na viwanda vingi vya kuchakata maparachichi na matunda mengine yanayolimwa katika mikoa mbalimbali, itasaidia pia wakulima kuwa na kasi katika kilimo.

Uchache wa viwanda vidogo, kwa namna moja au nyingine, unachangia matunda mengi kuoza mashambani au sokoni na kusababisha hasara kwa wakulima na wafanyabiashara.

Hivyo, kwa mtazamo wangu ni kwamba, viwanda vingi vya kuchakata matunda vijengwe vya kutosha ili kuwa suluhisho la hasara ya miaka nenda miaka rudi ambayo wakulima wa matunda wamekuwa wakiipata.

Nakubaliana na hatua zinazochukuliwa na serikali zitakazosaidia kutatua kero ya wananchi kuingia hasara kwa kutupa matunda hayo baada ya kuoza,

wakati serikali ikiendelea na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwanyanyua wakulima wa matunda, basi wakulima wenyewe hawana budi kuendelea kujiimarisha, kwa ajili ya soko la nje.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Watanzania tunamuenzi Mwalimu kwa matendo?



Pascal Mayalla

Karibu tena katika safu hii ya "Kwa Maslahi ya Taifa". Leo safu hii inaendelea kumuenzi mwasisi wa taifa hili, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kutokana na kumbukizi ya Baba wa Taifa kila Oktoba 14, ni Nyerere Day, nikitafakari jinsi sisi Watanzania, tunavyomuenzi na kuuliza je, tunamuenzi kweli kwa mawazo maneno na matendo au?

Wiki iliyopita niliishia nikiwa hosteli za Chuo cha Uandishi wa Habari (TSJ) enzi hizo kikiwa Ilala Sharif Shamba, nikapata ugeni wa kutembelewa na mtoto wa Mwalimu, Madaraka Nyerere, kunijulisha kuwa nahitajika nyumbani, Msasani kwa Nyerere!

Kwanza nilishtuka! Iweje mtu 'nobody' nihitajike nyumbani kwa Rais, kuna nini? Ndipo Madaraka akanieleza mdogo wake wa kike, amepata mchumba, hivyo familia imenipendekeza mimi kuwa mshereheshaji kwenye sherehe ya harusi ya binti Nyerere.

Nilipokea wito huo kwa furaha. Sikukumbuka hata kumuuliza Madaraka nani aliwaelekeza kwangu? Nikakubali moja kwa moja na kuulizwa gharama zangu. Kikweli siku hizo wala sikujua MC huwa analipwa, hivyo nikasema nitafanya bure!.

Nikarudi hosteli kuvaa suruali, maana nilitoka na bukta tu. Nilidhani ni wale wageni wetu wa ujana hosteli. Nikapanda 'sport car' hadi nyumbani kwa Madaraka, enzi hizo akikaa yale maghorofa ya SIDO. Ilikuwa siku ya kikao cha mwisho, harusi ni Jumamosi inayofuata. Safari ya Msasani ikaishia Upanga, kila kitu kimekamilika hakuna haja ya vikao! Tena sikumbuki kama huyo binti alifanyiwa 'send off', ila mimi ni MC wa harusi, kama alifanyiwa siwezi kujua, maana sikualikwa na sikuuliza.

Siku ya siku ikafika, harusi ikafungwa kanisa la KKKT Azania Front, sherehe ni ukumbi wa Luther House, karibu sana na hapo kanisa kuu la KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Sikumbuki hata kama kulikuwa na msafara!

Tumetoka kanisani ukumbi ni hapo hapo, tukaingia ukumbini, baada ya kutamani sana kumsalimia kwa kumshika mkono Mwalimu, siku hiyo ndiyo nikamshika mkono. Mwalimu alikuwa mtu mcheshi sana na ana vichekesho sana, akaniambia MC, usilete habari za uongo uongo ili kuwafurahisha wageni. Sipendi utani utani, endesha shughuli vizuri iishe mapema.

Kwanza nilikuwa 'very tense' kuendesha shughuli ya mtoto wa Rais. Baada ya kumsalimia Mwalimu kulikuwa na utulivu. Kwa jinsi sherehe hiyo ilivyokuwa, binti wa Rais ameolewa na mtu wa kawaida tuu, Baba wa bwana harusi ni Baba Mchungaji wa KKKT, hivyo sherehe ilikuwa ya kawaida sana, haina makuu yoyote.

Funzo hapa ni Mwalimu hakuwalea watoto wake kwa umuhimu wowote kama watoto wa Rais, hivyo kijana wa kawaida tu akampenda mtoto wa Rais, harusi ya kawaida sana. Hiyo ni kuonyesha Mwalimu alikuwa mnyenyekevu, mwenye kujishusha na aliyejiweka kuwa mtu wa kawaida sana. Nilipata bahati pia ya kuwa MC harusi ya Binti Lowassa, wakati huo Lowassa ni Waziri Mkuu. Nikilinganisha harusi ya binti Nyerere akiwa ni binti wa Rais na harusi ya binti Lowassa akiwa ni binti wa Waziri Mkuu, kiukweli kabisa ni kama mbingu na nchi!

Nikiwa bado TSJ, nilihudhuria kila mkutano wa Mwalimu na waandishi wa habari, hivyo ile mikutano ya Kilimanjaro Hotel na ule ya uzinduzi wa kitabu cha "Nyufa" nilikuwapo. Nilipomaliza TSJ nikaajiriwa RTD na nikam- 'cover' sana Mwalimu kwenye matukio na shughuli zake.

Mimi ndiye mwandishi wa mwisho wa habari kusafiri na Mwalimu safari ya Uswisi kwenye mkutano wa Tume ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini (South South Commission) uliofanyika jiji la Bern. Kwa hiyo mimi ndiye mwandishi wa mwisho wa habari kufanya mahojiano na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere niliyoyafanyia jengo la 'The Bundes House', mjini Bern. Baada ya kurejea kutoka Uswisi, ndipo akaanza kuugua.

Mwalimu alipozidiwa na kupelekwa kutibiwa katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London nchini Uingereza, ni mimi tena ndimi mwandishi pekee wa Tanzania, niliyemtembelea hospitalini hapo nikiwa pia mwandishi pekee wa Tanzania kutoka chombo cha habari binafsi. Niliandamana na Rais wa wakati huo, Benjamin Mkapa ziarani Marekani kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA). Wakati wa kurejea nchini, tukapitia London kumwona Mwalimu na kurejea nyumbani na baada ya hapo, haikupita wiki, Mwalimu akafariki dunia.

Niliandaa 'documentary' ya msiba, tangu kuwasili kwa mwili, kuagwa Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Uhuru), nikamsindikiza mpaka Butiama kwenye makao yake ya milele.

Swali la kumhusu Mwalimu, je, viongozi wetu wanamuenzi kwa kumuishi au wanamuenzi kwa mawazo tu na maneno lakini si kwa vitendo?. Naomba mnitajie hata kiongozi wetu mmoja tu anayemuishi Nyerere kwa mawazo, maneno na matendo.

Je, chama alichokiasisi na kukiacha Mwalimu Nyerere - Chama cha Mapinduzi (CCM), kinamuenzi Mwalimu kwa vitendo?, kinamuishi kwa kufuata falsafa yake? Je, hii CCM ya sasa ndiyo ile CCM aliyoiacha Mwalimu?

CCM ya Mwalimu ilikuwa chama cha wakulima na wafanyakazi. Sifa ya kugombea uongozi ilikuwa uwezo wa uongozi na uzalendo wako kwanza kwa nchi yako, kisha kwa chama chako. Je, sasa sifa za kuchaguliwa kuwa kiongozi CCM bado ni zile zile au sasa ili kuchaguliwa kiongozi sifa kuu ni uwe na mkono mrefu kiasi gani kuwapatia takrima wajumbe?

Mwalimu aliichukia rushwa kwa dhati. Baada ya kufariki dunia, tukaibariki rushwa kwa kuipa jina zuri la "takrima" tukapitisha na sheria kuiruhusu. Kelele zikapigwa, sheria ile ikafutwa, lakini sasa chama alichokiasisi Mwalimu zile takrima zimegeuzwa ni michango ya lazima ya kuombea fomu ya uongozi.

Kwa sasa fomu ya kugombea ubunge CCM inauzwa kwa Sh. milioni moja. Kuna wakulima wangapi na wafanyakazi wanayo hiyo milioni moja ya kujaza fomu ya ubunge? Mwalimu angekuwapo haya yangefanyika?

CCM, serikali yetu, viongozi wetu na Watanzania kwa ujumla, tumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, si tu kwa mawazo na maneno, bali kwa matendo na ikibidi kumuishi. Kwa hapo tutabarikiwa na taifa litabarikiwa.

Tukiendelea kumuenzi hivi kwa mawazo tu na maneno, lakini matendo ni tofauti, taifa letu na chama chetu na viongozi wetu, tutaendelea kupata kichapo cha bakora za kitu kinachoitwa karma.

**Wasalaam.**

**Paskali**
**+255 754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Ni karne ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Burito!



Na Joseph Kulangwa

APRILI 13, 1922 hadi Oktoba 14, 1999; hiyo ni miaka 77 aliyojaaliwa kuishi duniani Julius Nyerere, mjukuu wa Burito, akizaliwa Butiama, Mara na kufariki dunia London, Uingereza.

Ni miaka 23 tangu Mwalimu Nyerere aage dunia na kama angekuwa anaishi leo, ungekuwa mwaka wake wa 100, angekuwa anakula chumvi ya karne moja duniani.

Lakini Mungu kwa makusudi yake, akaona ni vyema amwite mbele ya haki na bila shaka huko aliko, anatuangalia Watanzania tunavyohangaika, kuneng'eneka na kudemka na hii nchi yetu na dunia kwa ujumla.

Juzi tuliadhimisha kitu kinaitwa Siku ya Nyerere na Waswahili hurahisisha na kuiita Nyerere Dei, wakiitumia kufanya sherehe mbalimbali huku wakiwa wamepumzika, hawaendi kazini, kwa sababu ni Siku ya Nyerere.

Ukizama sana ndani ya siku hii, unaweza kuona kasoro fulani hivi ingawa kwa mbaali. Lakini ukiikalia sawa ingawa utaweza kulaumiwa na wasiotaka mabadiliko, utaamini siku hii haikustahili kuitwa hivyo.

Utabaini, kwamba kumbe leo ingekuwa siku ya Watanzania kujikalia kimya majumbani tukimkumbuka Baba yetu wa Taifa, badala ya kufanya matamasha na sherehe kedekede zikiwamo za kukamua kinywaji, kumwagilia nyoyo.

Siku zote mimi huona na kushuhudia watu wakitumiana salamu za furaha zikihusisha Siku ya Kuzaliwa ambayo Waswahili kwa kutamba huiita Hepi Besi Dei (HBD), lakini sijapata kuona salamu za Hepi Desi (Death) Dei (HDD). Unadhani ni kwa nini? Kifo kinaogopwa au ni uchuro kumtakia heri mtu siku ya kifo au kufiwa? Ukipata jibu katika swali hilo, ujue sasa unapaswa kufikiria kwa nini tunaadhimisha Siku ya Nyerere Oktoba 14, yaani leo, na si Aprili 13? Kumbe kuna haja ya kukaa hata bila kupitia Kikosi Kazi, kutafakari kama tuko sawa na siku hii.

Yawezekana wakawapo watu wa kufikiria, kuwa huenda wazo hili ni la kijeuri tu halina mashiko, lakini naamini lina mashiko, kwa sababu ya umuhimu na uzito wa siku yenyewe, kwamba ni ya kifo cha mtu, hivyo kustahili shamrashamra kama siku ya kuzaliwa? La hasha!

Hilo somo linaweza kueleweka kwa wanafunzi wanaoelewa haraka, lakini kwa wale wenzangu wadadisi, itachukua muda mrefu kuingia akilini na kukaa sawa na kuona uzito uko wapi, lakini si lazima.

Lakini pamoja na yote hayo, hebu tunaposherehekea na kufurahia siku hii leo, je ni kweli tunamuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa aliyoyafanya akatuachia, au bora siku hii iwepo na ipite tusubiri mwakani?

Watanzania wakati tunaadhimisha Siku hii, tunapaswa kutafakari ni yapi mema aliyofanya Mwalimu Nyerere na akatuachia mwaka 1999, na ni yapi tuyaendeleze kwa mustakabali mwema wa Taifa letu.

Leo hii, ukienda mataifa ya nje husan haya ya jirani, Mwalimu anakumbukwa na kuenziwa pengine kuliko hata sisi ambao kumuezi kwetu, kumesalia kwenye kuyapa majina yake maeneo na miradi tu, na si fikra na matendo yake.

Tunashuhudia masikini wanavyozidi kuwa masikini huku matajiri wakielea kwenye ukwasi, tunaona ufisadi unavyotamalaki, huku vijana wetu wengi wakiendelea kusota mitaani bila ajira licha ya usomi wao.

Tunahanikiza kuhusu kujiajiri, kana kwamba ni kazi ya kufumba na kufumbua macho tu ajira zipo, watu kujiajiri na kuajiri wenzao. Viongozi wetu wako mstari wa mbele kuyahanikiza hayo.

Nyerere na wenzake enzi hizo waliweka utaratibu wa kuwatafutia vijana majukumu ya kufanya ili kuzalisha mali. Vijana waliokuwa wakizurura mitaani waliondolewa kistaarabu na kupelekwa mashambani kuzalisha.

Enzi za Gezaulole, Mwanadilatu, Kibugumo, vijana walipatikana huko wakiwa mashambani wakizalisha mali na kuacha kuzurura mitaani. Leo tunawasomesha na kuwaacha mitaani, wanapogeuka panyarodi tunalia vilio vya mbwa.

Nyerere na wenzake enzi zao waliona nuksi sana kwa viongozi kujilimbikizia mali, huku wananchi wa kawaida wakisota kwa ufukara unaonuka, leo hii kiongozi kuwa na mali ni sifa tena ya kupewa jukumu la kuongoza masikini!

Hata kama ya Nyerere na wenzake yalifanywa zamani na kuona sasa yamepitwa na wakati, lakini bado tuna nafasi ya kuona mema yake na kuyatekeleza na kuyaendeleza, ili hata vizazi ambavyo havikumwona, basi vimhisi kuwa alikuwapo babu aliyefanya haya na sasa yanatusaidia.

Jamani, Nyerere Dei njema. Alamsiki!

***kulangwasos@gmail.com**

# WB yaimwagia sifa Tanzania usimamiaji mzuri wa uchumi

**Na Mwandishi Wetu,**
WASHINGTON D.C

BENKI ya Dunia (WB) imeimwagia sifa Tanzania kwa usimamizi mzuri wa uchumi na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayopata fedha kutoka kwenye taasisi hiyo kulinganishwa na nchi zingine nyingi za Afrika.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia anayesimamia Kundi la Kwanza la Nchi za Kanda ya Afrika (Africa Group 1 Constituency), Dk. Taufila Nyamadzabo, alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Tanzania jijini Washington D.C, Marekani.

Ujumbe huo unaoongozwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba kwenye Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Dk. Nyamadzabo alisema Tanzania ni nchi ya mfano katika usimamizi wa uchumi ambapo licha ya majanga mbalimbali, ikiwamo UVIKO-19 na vita inayoendelea baina ya Urusi na Ukraine, tathmini inaonyesha uchumi wa Tanzania uko imara na nchi inakopesheka.

Aliahidi kuwa benki yake itaendelea kuisaidia Tanzania katika jitihada zake za kukuza uchumi na kuwaondolea umaskini wananchi wake kwa kusaidia rasilimali fedha zitakazotumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu, alimweleza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia huyo kwamba uchumi wa Tanzania unazidi kuimarika na serikali itaendelea kuchukua hatua muhimu kuhakikisha unazidi kuimarika na kuleta ahueni kwa wananchi.

Alifafanua kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 uchumi umekua kwa asilimia 5.4 kulinganishwa na ukuaji wa asilimia tano katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha uliotangulia (2021/22) na kwamba kutokana na mipango kabambe iliyowekwa na serikali, uchumi utakua zaidi hadi kufikia wastani wa asilimia 6.3.

Dk. Mwigulu alirejea shukrani zake kwa Benki ya Dunia kwa kuitengea Tanzania jumla ya dola za Marekani bilioni 2.1 sawa na Sh. trilioni 4.9 katika mzunguko wa 20 wa IDA (Julai 2022-Juni 2025) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotarajiwa kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na kupunguza umaskini wa watu wake.

Mpaka sasa Benki ya Dunia imewekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 7.2, sawa na takriban Sh. trilioni 16.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi zaidi ya 29 nchini.

Kati ya miradi hiyo, 24 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 6.41 ni ya kitaifa na mingine mitano yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 0.75 ni ya kikanda.



Diwani wa kata ya Majengo, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Mukadam Sabuni, akiwaongoza vijana wa UVCCM, kuchangia damu katika kituo cha Afya cha Ubwari juzi, ikiwa ni sehemu ya kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwenye kofia ni Mwenyekiti wa CCM wilaya hiyo, Laick Gugu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yatenga mashamba mradi wa vijana wa kilimo

**Na Renatha Msungu,**
CHAMWINO

SERIKALI imetenga ekari 93 za mashamba katika mikoa ya Mbeya na Dodoma kwa ajili ya kuendeleza mradi wa vijana wa kilimo biashara ambao utawasaidia kujiinua kiuchumi, ikiwemo kujiajiri pindi wanapohitimu masomo yao.

Serikali inatarajia kutumia Sh. bilioni 230 kwa ajili ya kutengeneza mradi huo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji na ujenzi wa maghala.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya kukagua mashamba pamoja na maandalizi ya mradi wa kilimo wa vijana wilayani Chamwino mkoani Dodoma.

Bashe alisema ekari hizo za mashamba katika mikoa hiyo zinatarajiwa kutengeneza ajira mpya 18,000 ambazo zitatokana na mradi huo wa kilimo ambao utaendeshwa katika mikoa hiyo ya Mbeya na Dodoma.

Bashe alisema vijana wengi wamekuwa wakikosa miundombinu wezeshi ambayo itawasaidia kwa ajili ya kujiinua kiuchumi, hivyo ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji itawasaidia kuendesha kilimo ambacho kitawafanya wakopesheke.

"Wizara imeamua kutenga maeneo haya ili kuhakikisha vijana wanakopesheka kwa ajili ya kujiinua kiuchumi kupitia kilimo," alisema Bashe.

Waziri huyo alisema mradi huo wa vijana unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 230 ambazo zitatumika katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na ujenzi wa maghala ambayo yatatumika katika mradi huo wa kilimo.

Alisema katika hilo, serikali inatarajia kushirikiana na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA) ili kuhakikisha wanafanikisha mradi huo.

"Katika hili tutashirikiana na AGRA ili kuhakikisha serikali inafikia malengo iliyojiwekea katika kilimo kwa upande wa vijana," alisema Bashe.

Alisema suala hili litawasaidia vijana wanapohitimu masomo yao kujikita katika kilimo hususani pale wanapokuta miundombinu imeboreshwa na serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali.

Rais wa taasisi hiyo, Dk. Agnes Kalibata alisema watashirikiana na serikali katika mradi huo ili kuwapa fursa stahiki vijana ambao ndio walengwa wa mradi huo.

Dk. Kalibata alisema mradi huo unategemewa kumaliza tatizo la ukosefu wa chakula nchini, ukihusisha kuandaliwa kwa vijana katika kilimo biashara ili kuzalisha chakula cha kutosha na kuuza ndani na nje ya nchi ili kujiinua kiuchumi.

## Mbunge aishauri serikali kuwatambua wakimbizi

**Na Halfani Chusi**

Mbunge mstaafu wa Kasulu, Daniel Nsanzugwauko ameishauri serikali kuwatambua wakimbizi kulingana na taaluma zao ili nchi ifaidike nao.

Vilevile, amesema wakimbizi siyo watu wa ovyo kama jamii inavyoamini, akibainisha kuwa kati yao, wapo wenye taaluma na vipaji ambavyo vinaisaidia nchi katika maeneo mbalimbali.

Kiongozi huyo alitoa ushauri huo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla iliyoandaliwa na Shirika la Dignity Kwanza kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahariri wa vyombo vya habari namna ya kuripoti habari hizo.

Alisema kupakana kwa Mkoa wa Kigoma na nchi nne za ukanda wa Afrika (Rwanda, Zambia, DRC na Burundi) ndiyo sababu kuwapo kwa wakimbizi wengi maeneo hayo.

"Wakimbizi wengi wapo katika mkoa huo kwa sababu ukiwa Kigoma kwenda katika nchi hizo, hakuna umbali mrefu, hazifiki hata Km 22.

"Kwa hiyo, mkoa ule una wakimbizi wengi sana na mimi nimekuwapo huko kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ninaielewa vizuri jiografia ya kule.

"Ukiwaangalia wakimbizi wengi walioko huko, wengine wamekuwapo tangu enzi za Rais wa Awamu ya Kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wamesoma hapa, wana wajukuu na tunafanya nao shughuli za kijamiii kama Watanzania wenzetu lakini sio raia

"Kwa mfano, mafundi umeme wengi waliopo Kigoma ni wale waliokuwapo katika kambi ya wakimbizi Nyalususu, lakini ndani yao kuna watu wenye taaluma mbalimbali, wengine ni wahandisi. Watanzania kwa ujumla hatupaswi kuwatazama katika mitazamo hasi," alisema.

Alifafanua kuwa wakimbizi waliopo nchini wamekimbia nchi zao kwa kuhofia kifo, hivyo wako hapa kwa ajili ya kulinda usalama wao na wanapaswa kupewa haki kama raia wa Tanzania na sio kunyanyapaliwa.

Aliiomba serikali kuwapatia uraia wakimbizi waliokaa nchini kwa muda mrefu, akisistiza kuwa wale ambao hawatakuwa tayari, iangaliwe hali ya nchini kwao warudishwe kuliko kuishi na watu wasio na uraia.

"Serikali iwaite ikae nao, iwatambue baada ya hapo iongee nao ili wale wanaotaka kubakia hapa nchini wafuate taratibu za kisheria wapewe uraia, wasiotaka basi warudishwe katika nchi zao maana wanavyozidi kutapakaa nchini, baadaye yanaweza kutokea machafuko makubwa," alitahadharisha.

Mkufunzi kutoka Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSMO, Khoti Kamanga alisema serikali inapaswa kuendelea kuenzi sera alioiacha Mwalimu Nyerere ya kutowabagua wakimbizi.

"Sera aliyoiacha Nyerere inasema 'Ukarimu na milango wazi kwa watu wanaokuja kutafuta hifadhi', ukiitazama mantiki ya sera hii utagundua kuwa ilikuwa imelenga kuwasadia hifadhi watu ambao nchi zao zipo katika machafuko kwa wakati huo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Dignity Kwanza, Janemary Lukumba alimsifu Mwalim Nyerere kwa kutoa hifadhi kwa wakimbizi enzi za uongozi wake, kulikompa tuzo maalum ya kuthamini wakimbizi

"Katika kumbukizi ya kifo chake tumeona tukumbuke pia mchango wake na maono yake kuhusu wakimbizi, maono yake bado yanaishi mpaka leo," alisema.

# MAISHA

OKTOBA 16, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 15



## Boresha uso wa mbele ya nyumba mara kwa mara



Ukurasa 14

## KASHATA ZA UFUTA



## SURUALI PANA ZINANOGA


Ukurasa 13




# KUWA ANGAVU BILA MKOROGO

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | S | H | A | K | A |
| | H | | | O | |
| L | I | A | | K | |
| | N | | T | O | A |
| | D | | | T | |
| T | A | M | B | O | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UMA, SANDA, TAMKO, KANDIA, TAMBUA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



MTOTO Juma alikwenda kwa babu yake shambani kwa ajili ya kumsalimia. Alipofika alimkuta babu yake akiwa shambani anapalilia mahindi.

Juma alikwenda kule alipokuwa babu yake na kumsalimia, alipomaliza alimwambia anataka kumuuliza kitu.

Juma: Babu kwani, mtu ukitaka mali lazima ulime shamba?

Babu: Hapana mwanangu, wapo wanaopata mali kwa kufanya biashara au kufanya kazi ofisini.

Juma: Mbona mwalimu alituambia kama tukitaka mali tutapata shambani?

Babu: Mjukuu wangu huo ni msemo tu unaotuhimiza kufanya kazi kwa bidii ili tupate mafanikio.

**SWALI**

Taja wanyama jamii ya sokwe ambao unawafahamu.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mama alimsomesha akawa daktari, anamkana mbele ya walinzi hamjui

KARIBU tena msomaji tuendelee na sehemu ya tatu ya simulizi inayowahusu wale wanaodharau na kusahau wazazi wao. Tunavyoendelea na simulizi hii, mwishoni utaona laana iliyompata daktari aliyesomeshwa na mama yake lakini alipofanikiwa akamdharau.

Kwa wale ambao hawakufuatilia, wiki iliyopita niliishia pale mama alipotoka kijijini na kuelekezwa anakoishi binti yake ambaye ni daktari huku wakiwa wamepotezana kwa miaka takriban 14 bila kuonana.

Hata mama alipofanikiwa kufika nyumbani kwa bintiye huyo, alijikuta anafukuzwa kiaina. Mama alifika na kupokewa na walinzi wa nyumbani kwa daktari. Binti alipofika na kujulishwa akamwambia hamjui na wala asimguse.

Mama alijitahidi kumkaribia kwa furaha, binti akamwambia sina mama wala baba. Ndipo mama akabaki anashangaa nini kimemsibu bintiye. Daktari akaendelea na shughuli zake wala hakumkaribisha mama yake. Mama akatafuta sehemu akakaa chini kwa kuishiwa nguvu, akatafakari sana.

Mama akamwomba Mungu amsamehe asije akawaza mengine yakampata mabaya binti yake. Mama akaanza kuomba toba akasema " Mungu naomba nisamehe maana naona anakoelekea binti yangu si kuzuri. Nisamehe mimi ndiyo tumbo langu lililomleta duniani.

"Kama kwangu mimi niliyembeba tumboni miezi tisa amefanya hivi leo, sijui kama huko kwa wengine anawafurahia, anawalisha vizuri lakini leo haya ananifanyia mimi." Mama akawaza na machozi yakamtoka. Alilia amekaa kwa takriban saa moja hivi ili aamini kwamba je, ni kweli au si kweli. Walinzi wale wakamwambia mama si tulikuambia bosi wetu hana baba wala mama. Labda ungesema ni ndugu tu umekuja kuomba msaada.

Dada akajifungia ndani, mama mzazi yuko nje. Alihuzunika sana. Akawaambia wale vijana walinzi nawashukuru, sasa acha niondoke. Wakamsihi sasa unaenda wapi? Akawaambia nyie sikilizeni maagizo ya bosi wenu, acha niende kwetu!

Ni kama binadamu mama lazima ajisikie uchungu kwa kuona ile hali ilivyoendelea pale. Fikiria mama aliyemzaa yule binti alipata uchungu kiasi gani kwa kujibiwa majibu kama yale.

Ni miaka 14 imeisha hakuwahi kuonana na binti yake, leo anamwona lakini hamtaki. Anatamani amkumbatie lakini wapi! Anatamani afurahi na mwanawe lakini anamwambia usiniguse, sina mama wala baba.

Ana mali za kutosha, ni daktari na anaona mama si wa hadhi yake. Kumbe angeweza kumchukua na kumbadilisha awe na maisha mazuri vile atakavyo yeye, ingewezekana kabisa! Lakini alishasema kwa marafiki zake hana wazazi. Na hata kama angemchukua angemtambulishaje. Je, ni mama mdogo au shangazi?

Yule mama akageuka nyuma wakati anaondoka, akaona kanisa jirani na pale akaingia mle ndani. Akaanza kuomba kama vile alikuwa anasikitika. Upo wakati unapofikwa na jambo na unapotamani kuomba unakuta huzuni inatawala.

Unakuta unalia tu kwa kububujikwa na machozi. Unaweza kusema ni nguvu ya Mungu imeshuka kumbe ni machozi ya uchungu wa moyo. Mama akalia kwa dakika nyingi baadaye akamjia Mchungaji wa kanisa lile ambaye ndiye aliyetoa kisa hiki.

Mchungaji na huyo daktari wanaishi jirani kabisa, wanafahamiana vyema. Mama alipomaliza kuomba wakasalimiana na Mchungaji, wakaenda ofisini. Ndipo Mchungaji akapata habari nzima ya kisa hiki.

Mchungaji aliumia sana kwa nini binti amfanyie mama yake hivyo? Akamwambia mama kuwa yeye alimzika mama yake miezi miwili iliyopita na kumwomba achukue nafasi ya mama yake mazazi. Akamwambia, wewe uwe mama yangu. Mimi ni mtumishi wa Mungu tu hapa, natamani mama yangu angekuwapo. Kwa nini binti afanye hivyo?

Ni pepo gani limemwingia hata kumkataa mama yake kwa kiwango hiki! Anamwacha aondoke ni usiku, ametoka kijijini na hamjui mtu mjini na hata aliyemleta na kumwacha getini kwa bintiye, aliondoka hajui anakoishi.

Yeye binti ana amani, amejifungia ndani. Mchungaji alitamani aende abishe aongee naye lakini mama alimzuia akamwambia, wewe ni kama mwanangu, naomba usiende, mwache! Maadam ana amani moyoni mwake, sina neno ila namwomba Mungu anisamehe lisije likampata baya binti yangu.

***Mpenzi msomaji, kile alichotarajia sicho alichokikuta. Aliona kama ndoto. Ama kweli, Maisha Ndivyo Yalivyo! Wiki ijayo; Mama baada ya kuongea na Mchungaji aliondoka usiku ule. Nini kilimtokea? Je, una maoni au kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Athari za mabadiliko ya tabianchi ni maumivu kwa wengi

MOJA ya matatizo makubwa yanayoikabili dunia na Tanzania ikiwamo, ni kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha kukosekana kwa mvua za kutosha, kuwapo ukame, mafuriko na madhara mengine yanayotishia uhai wa watu.

Mabadiliko ya tabianchi hayasababishwi na eneo fulani pekee bali mchango wa dunia kwa ujumla, huku nchi za Afrika kwa ujumla wake, zikichangia hewa ukaa chini ya asilimia nne huku nchi zilizoendelea zikichangia kwa kiasi kikubwa.

Mathalani, kwa Tanzania mtu mmoja anachangia gesi ukaa kwa asilimia 0.22 kwa mwaka, huku China na Marekani akichangia asilimia 26 kwa kipindi hicho hicho kutokana na shughuli za viwanda na nyinginezo ndiyo maana nchi hizo zinatoa fedha za kusaidia kukabili kwa nchi zilizotunza mazingira.

Hadi sasa hakuna mpango kwa nchi hizo kupunguza viwanda, ndiyo kwanza vinaongezeka na ziko tayari kuendelea kutoa fedha kwa nchi zinazochangia kupunguza hewa ukaa kwa kutunza mazingira.

Kwa sasa kila eneo linakabiliwa na ukame huku maji ambayo ni muhimu kwa kila kiumbe yakiendelea kupungua, migogoro baina ya binadamu na binadamu; wanyama na binadamu inaongezeka kwasababu raslimali hiyo inapotea baadhi ya maeneo.

Ukisafiri kwa anga utaona hali ilivyo ardhini, lakini kasi ya kupaa kwa bei ya nafaka kulikochagizwa na kupaa kwa bei ya mafuta ni udhihirisho kwamba ukame ni tishio, pia unaona mito na maeneo mengine yalivyokauka.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilieleza mwelekeo wa mvua kuwa si wa kuridhisha na wakulima wameshauriwa aina za mazao ya kulima ambayo ni ya muda mfupi na yenye kuhimili ukame.

Tunapoelekea kwenye mkutano wa wakuu wa nchi kuhusu mabadiliko ya tabianchi COP27 utakaofanyika Cairo, Misri, ambao pamoja na mambo mengine kila nchi itaeleza ilivyotekeleza mpango wa kukabili mabadiliko hayo na afua zilizochukuliwa, ni muhimu kujitathimini kama nchi namna ya kuhakikisha kila kiumbe hai kinaendelea kuishi kwa wakati huu.

Hadi sasa tunaona uhaba wa nafaka huku ikizidi kupanda bei, ongezeko la migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambao wanatoka maeneo yaliyohifadhiwa kwenda kutafuta malisho, huku binadamu nao wakivamia maeneo ya hifadhi kupata mahitaji ya Wanyama wafugwao.

Jitihada nyingi zimefanyika ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira, kupanda miti kwa wingi na kuachana na matumizi ya nishati ya kuni, ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa mkaa unatumika zaidi kutokana na kupaa kwa bei ya gesi.

Hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu sana kwa sasa, nafaka zimepanda bei hali ya maisha inakuwa ngumu kutokana na visababishi vingine kama kupanda kwa bei ya mafuta na COVID-19.

Mabadiliko ya tabianchi si jambo la kulichukulia rahisi, lazima nchi iendeleze mikakati yake ya kusaidia wananchi wake kuishi na hali hiyo ambayo haiwezi kuisha leo wala kesho kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Lazima jamii yetu iendelee kuelimishwa namna ya kutumia fursa katikati ya matatizo, mathalani kwa sasa kuna biashara ya hewa ukaa kwa wananchi waliotunza misitu ya asili,misitu ya kupanda na binafsi ambayo wanauza duniani kwa nchi zilizoharibu au zinazoharibu mazingira.

Misitu hiyo inasaidia kupunguza hewa ukaa kwenye anga na kukabili hali iliyopo sasa ya vipindi vya mvua kutoeleweka,ukame wa muda mrefu, joto na baridi kali kiasi cha kuathiri binadamu na viumbe wengine. Kama tunavyoona sasa maeneo mengi yana joto kali hadi misitu inawaka yenyewe na kwingine baridi sana.

Kwa sasa usalama wa chakula uko hatarini kwa kiasi kikubwa,kwamba wananchi hawana uhakika wa mlo kamili kutokana na kwamba hawana uhakika wa chakula chenyewe ili waendelee kuwa hai.

Hivyo, kupambana na mabadiliko ya tabia nchi ni lazima kwa kila mmoja lakini wananchi kutumia mbinu zao na za jumla kukabili hali hii,ili dunia iwe salama kwa kila mmoja anayestahili kuifurahia.

Kwa sasa tunasikia migogoro baina ya wanyama na binadamu inashamiri,wanyama wanatoka kwenye maeneo yao ya asili kutafuta malisho na binadamu anapeleka mifugo maeneo yaliyohifadhiwa kutafuta malisho,hii inafanya maisha yasiwe na amani kwenye maeneo mengi.

Mabadiliko ya tabia nchi ni tishio lazima tuwe na mbinu zinazotekelezeka,kubuni namna ya kuendelea kupata maji ya mahitaji ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji kwasababu cha mvua hakijaonyesha manufaa chanya.









Unaweza kutoka tofauti kwa kuvaa mavazi ya kiafrika wakati wa harusi. Pichani ni baadhi ya mitindo ambayo inapendeza kuvaliwa wakati wa ufungaji wa ndoa.

MITINDO



# SURUALI PANA ZINANOGA



MTINDO wa kuvaa suruali pana unazidi kushika kasi kwa watu wote. Hii sio kwa wasanii maarufu pekee, bali umeanza kupendwa na watu wa ngazi zote.

Katika kipindi hiki cha joto, suruali pana zina umuhimu wake, licha ya kuongeza uzuri wa mwonekano, pia husaidia kuuweka mwili katika hali bora.

Hata hivyo, wengi hawajui namna ya kupangilia vazi hili hasa aina ya viatu unavyotakiwa kuvivaa ili kukupa matokeo mazuri zaidi.

Wataalam wa mavazi wanashauri si kila aina ya viatu vinafaa kuvaliwa na nguo hizi, bali kuna viatu vichache ambavyo vinapendeza zaidi pale unapovalia na suruali pana.

Suruali pana na 'sneakers'

Suruali pana laini na inayofanana na nguo za michezo, ni vyema ukavalia na viatu vya aina ya raba maarufu kama 'Sneaker'.

Mpangilio huu unakupa mwonekano wa kuvutia, mara nyingi inakuonyesha kama mtu unayejijali kiafya na mpenda mazoezi ya mwili.

Suruali pana na visigino virefu

Kama wewe unapenda mialiko na shughuli inayowakutanisha watu mbalimbali, kumbuka utapendeza kama ukivaa suruli pana ya kitambaa laini na kiatu cha kisasa chenye visigino virefu.

Unapovaa suruali ya aina hii pamoja na shati la kubana linaloonyesha mikatiko ya kiuno vyema, viatu vya visigino virefu vitakupendeza kwa sababu itakupatia mwendo maridadi zaidi.

Suruali pana na Texans

Uvaaji wa suruali pana aina ya culotte ni chaguo zuri kama unataka kwenda katika hafla mbalimbali au sherehe za kijamii.

Hata hivyo, itakuwa vyema kama utavaa pamoja na viatu vya aina ya Texans nyeupe, kwani utaweza kujiweka katika utofauti zaidi.

URÉMBO

Na Mary Geofrey

# KUWA ANGAVU BILA MKOROGO



Wanawake wengi na baadhi ya wanaume wanatumia vipodozi vilivyo na kemikali ili waweze kubadili rangi ya ngozi na kuwa nyeupe.

Lakini leo nitakupa njia moja tu itakayoweza kukusaidia kuwa na rangi nyeupe bila kutumia vipodozi vyenye kemikali katika ngozi yako.

**Mahitaji**

1. Asali kijiko kimoja cha chai
2. Juisi (maji maji ya limau) kijiko kimoja cha chakula.
3. Maji ya uvuguvu

**Jinsi ya kutengeneza mchanganyiko**

Changanya juisi ya limau na asali katika chombo kimoja kisafi na uchanganye ukitumia uma au kijiko cha kawaida kwa dakika kadhaa.

Matumizi

Osha uso vizuri ukitumia sabuni (kama unapata sabuni ya habati soda inakuwa vizuri zaidi) na maji ya uvuguvugu kisha jifute na kitambaa kisafi.

Jipake mchanganyiko huo usoni na maeneo yote ya shingoni taratibu huku ukijipaka taratibu kwa dakika 10.

Osha uso kwa maji safi, mwisho jifute kwa taulo safi.

Hakikisha unafanya zoezi hili kwa wiki mara mara moja mpaka mara tatu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# KASHATA ZA UFUTA

MAPISHI ya kashata ni rahisi na unaweza kupika nyumbani kwako na ukafurahia na familia yako.

Unaweza kupika kashata hizi kwa muda mfupi lakini kutumia njia rahisi.

**Mahitaji**

Ufuta Kilogramu mbili na sukari nusu kilo.

**Jinsi ya kutengeneza**

Chukua ufuta peta na toa takataka zote.

Ukimaliza weka ndani ya sufuria yenye maji, osha na chekecha michanga kama unavyofanya unaposafisha mchele kutoa mchanga.

Chuja maji na uanike juani, ukikauka uukaange kidogo mpaka uniukie na kuwa rangi ya kahawia na kisha chukua sufuria weka sukari na ubandike jikoni.

Koroga mpaka sukari ilainike na uweke ufuta wako kisha geuza geuza mpaka ichanganyike na ishikane, ipua ufuta harakaharaka na uweke katika kibao cha kusukumia chapati au meza.

Chukua kisukumio paka mafuta na uanze kusukuma hadi litokee duara kama chapati, chukua kisu kikali kata muundo wa pembe nne au upendavyo na uache ukauke ukikauka utoe na uhifadhi tayari kwa kuliwa.

Ukitaka kufanya madonge ukishautoa tu jikoni nawa mikono yako anza kuviringisha vitonge huku ukiwa unauchovya mkono wako kwenye mafuta au maji kidogo ili sukari isinase mikononi.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Boresha uso wa mbele ya nyumba mara kwa mara

## Namna ya kuchagua taa za chumba cha kulala



TAA za chumba cha kulala ni vitu muhimu na kuna wakati zinakuwa kama sehemu ya mapambo ya kupendezesha chumba chako. Kuchagua taa nzuri kwenye vyumba vya kulala unatakiwa kuwa makini zaidi kwani kinyume chake unaweza kufifisha vyumba na kuonekana na mandhari mbaya.
Iwe ni chumba cha kulala cha vijana, watoto au watu wazima, taa kamili zinazotoa mwanga wa kupendeza ni suala linalotarajiwa. Hizi ni baadhi ya dondoo za namna ya kuchagua taa za kwenye vyumba.

1: Taa za chumba cha kulala cha kawaida
Hizi ni baadhi ya taa ambazo unashauriwa kuziweka kama hutaki madoido mengi, lakini hakikisha ziwe na mwanga ang'avu na zisizoleta ukakasi unapoingia chumbani.

2: **Taa za wicker**
Taa za wicker ni nzuri kuweka vyumbani japokuwa zinaonekana kama mtindo wa kizamani, lakini zinapendezesha na kuweka mwanga mzuri.
Kama unaweza kupata vikapu vyenye vitambaa maridadi, taa za wicker zitakupa matokeo mazuri, pia hazitoi joto kama zilivyo taa zingine.

3: **Taa za mtindo wa kisasa**
Huwezi kukosa mawazo ya kisasa ya kibunifu, na hata unapotaka taa za kisasa ni lazima uchague mitindo mizuri ambayo unaweza kushangaza watu wanapoingia ndani.
Taa hizi zitatoa mwanga hafifu kwa hivyo italazimika kuunganishwa na zingine ndani ya chumba cha kulala ili mwanga uwe wa kawaida.

4: **Taa za kunyongwa**
Taa hizi zina mitindo tofauti, kama unataka kwenye vyumba vyako ni lazima kuhakikisha unapata iliyobuniwa vizuri. Jambo la muhimu lazima ufikirie mahali unapotaka kuziweka kwani ni lazima ziwe juu na kama ukitaka ziwe ukutani ni muhimu kuweka ambazo zina mwanga wa kawaida.

MABORESHO ya nyumba ni jambo la muhimu katika kufanya makazi yapendeze na yavutie. Maboresho haya yanapaswa kufanyika mara kwa mara katika kuimarisha ustawi wake.

Mbali na kufanya maboresho kwa ajili ya kuiimarisha nyumba, pia huchangia kwa kiwango kikubwa iendelee kuwa na mvuto.

Msanifu Majengo, Hafidhi Juma, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha zaidi na kuweka tofauti uso wa mbele wa nyumba na maeneo mengine.

"Kuna nyumba zingine zimekosa mwonekano mzuri wa mbele, hivyo husababisha kushindwa kutofautisha uso wa mbele na wa nyuma wa nyumba au upande wa kulia na kushoto. Na hapa ndipo tunasema kwamba kuna haja kwa msanifu kutumia maarifa kuandaa ramani ambayo itakidhi mahitaji ya nyumba husika," anasema.



"Baadhi ya sehemu za mbele za uso wa nyumba ambazo ni muhimu kuzipendezesha ni nguzo ambayo ni sehemu ya jengo kwa kuiweka kuwa ya duara, mstatili au mraba na hii itategemea namna ilivyosanifiwa, lakini jambo la msingi ni kuhakikisha unatengenezwa kwa ustadi mkubwa," anasisitiza.

Pia anasema katika kutengeneza uso wa mbele wa nyumba ni vizuri kutumia malighafi ambayo ni rafiki na yanavutia macho, imara na ambayo haina madhara kwa binadamu.

"Hili linawezekana kwa sababu Wasanifu wanafahamu malighafi bora za kutumia katika kutengeneza eneo hili kwa hiyo ni vema kuwatumia ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima," anasema.


Mbali na nguzo, mtaalamu huyo anasema madirisha nayo ni eneo muhimu ambalo linapaswa kuwekewa urembo hususani lililoko mbele ya uso wa nyumba.

"Na katika kutengeneza dirisha la mbele la uso wa nyumba, hapa napo kutategemea na vigezo vya sehemu au sababu za kisanifu, Msanifu anatakiwa kutumia utaalam wake kupendekeza aina ya dirisha kulingana na malighafi anayotaka kuweka iwe ni kwa mlalo au unyoofu," anaongeza.

Eneo lingine la kuboresha kwenye uso wa nyumba anasema ni milango ya nje. Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, milango ya nje bila kujali aina zake, hutumiwa kwa kuzingatia aina ya mtiririko wa kisanifu ili kutokupoteza mnyororo mzima wa mtindo na mpangilio wa jengo ulivyo.

Hafidhi anashuri kwamba wakati maboresho au matengenezo yanafanywa kwa ajili ya kupendezesha uso wa mbele wa nyumba, ni vyema kutokusahau na uchaguzi wa rangi kwenye ukuta na dizaini katika varanda lake katika uso huo wa mbele wa nyumba.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA 2022
NA MUHIDINI MSAMBA
0656 122770 SMS
UZEMBE
...HADUBINI...
HILI DUBWANA NIKILEMAA LITANILIPUKIA LAZIMA NIONGEZE SPIDI
NILIKUELEZA USITUMIE PESA HOVYO ONA SASA TUNAISHI KWENYE MBAVU ZA MBWA!?
UKINIKUMBUSHIA HAYO UTANIFANYA NILIE HADI NIGALEGALE KAMA MTOTO
MBONA SIJAKUELEWA SHOGA!?
NIKWENDA KWA WAGANGA KUTAFUTA NDOA,HII BIASHARA ISHAKUWA SIO
KAMA KWA MUME WA MTU MGANGA ATA DUNDA
HILO TUMBO LINGEKUWA NANII INGEKUWA MIEZI MINGAPI!?
KAMA UMEKOSA LA KUONGEA BORA UNYAMAZE KULIKO KUTAFUTA UGOMVI!?
MKE WANGU ANANIPIGA SANA HADI NATAKA KUHAMA
STORI ZINGINE SIO MWAKE HUMU
HAJAPITA MKOLENI, SIO MAKOSA YAKE
UNANITIA AIBU RAFIKI
KWANI NINACHO ONGEA NI UONGO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
TUI LA NAZI LITABAKI KUWA TUI HALIWEZI KUWA MAZIWA

## HABARI KIMATAIFA



Askari wa wanyamapori akimpa mtoto wa Tembo maziwa yaliyoboreshwa kwa kutumia chupa wakati wa asubuhi katika hifadhi ya Wanyamapori ya Namunyak, Samburu, nchini Kenya. Wanyama hao wamekusanywa katika juhudi za kuwaokoa kutokana na ukame unaoendelea nchini humo. PICHA : AFP

# Rais Putin atangaza kupunguza kipigo, Marekani yaongeza msaada Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin amesema hakuna umuhimu wa kuendelea kufanya mashambulio makubwa nchini Ukraine kwa sasa.

Kauli hiyo ameitoa siku chache baada ya vikosi vyake kufanya mashambulizi makubwa ya mabomu nchini humo tangu vita hiyo kuanza.

Rais Putin, alisema shabaha nyingi zilizolengwa za mabomu hayo yamefanikiwa na kwamba haikuwa lengo lake kuiangamiza Ukraine.

Alisema nchi yake itatimiza lengo la kusajili wanajeshi wa ziada 300,000 ndani ya wiki mbili.

Kauli hiyo inakuja wakati vikosi vya Russia vikionekana kurudi nyuma huku vya Ukraine vikisonga mbele, karibu miezi minane tangu uvamizi huo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa kilele na viongozi wa kanda katika mji mkuu wa Kazakhstan Astana, kiongozi huyo wa Russia alisema kuwa mashambulizi ya hivi karibuni yamepiga maeneo waliyolenga 22 kati ya 29 yaliyowekwa na jeshi la Ukraine na kwamba wanamalizia saba yaliyobaki.

"Hakuna haja ya mashambulizi makubwa. Sasa tuna kazi nyingine," alisema.

Kuanzia Jumatatu Russia ilianzisha wimbi la mashambulizi katika miji yote ya Ukraine, katika kile Putin alisema ni kulipiza kisasi kwa mlipuko ambao uliharibu daraja muhimu kati ya nchi hiyo na eneo la Crimea.

Makumi ya watu waliuawa na kujeruhiwa katika mashambulizi hayo ambayo pia yaliharibu miundombinu. Maeneo ya kati ya mji mkuu wa Kyiv yalilengwa kwa mara ya kwanza tangu uvamizi huo.

Putin alisema haikuwa nia ya Russia kuiangamiza Ukraine, lakini hakujutia uvamizi huo.

"Kinachotokea leo si cha kupendeza, kuweka mambo kwa upole,lakini hata hivyo, kama Russia isingeshambulia tungekuwa katika hali sawa, hali ingekuwa mbaya zaidi kwetu. Kwa hiyo tunafanya kila kitu kwa usahihi na kwa wakati ufaao." Alisema Rais Putin

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alisema wanajeshi 220,000 wamehamasishwa kujiunga na jeshi kati yao 16,000 walikuwa tayari katika mapigano.

Aidha, alisema hakuona haja ya kuhamasishwa na kusajili wengine zaidi, aliongeza.

**WANAJESHI ZAIDI WAENDA BERALUS**

Kundi la kwanza la wanajeshi wa Russia ambao ni sehemu ya kikundi cha vikosi vya pamoja na Belarus wamefika nchini Belarus.

Wizara ya Ulinzi ya Belarus, ilisema wanajeshi hao waliwasili katika juhudi ya kulinda nchi hiyo dhidi ya mashambulizi kutoka nje.

Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko alitangaza kuundwa kwa kikundi cha wanajeshi wa kikanda Oktoba 10 mwaka huu.

"Kama ilivyosemwa tutaifanya iwe Daraja la Crimea la pili," Lukashenko alinukuliwa na wakala wa habari wa serikali (BelTA).

Kauli hiyo sio ya kwanza kwa Lukashenko kutoa maoni kwamba shambulio lilikuwa linatayarishwa kwa Belarus. Baada ya kutangaza kuundwa kwa kundi la wanajeshi wa Russia na Belarus.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky katika mkutano wa G7 alitoa wito wa kutumwa waangalizi wa kimataifa kwenye mpaka wa Belarus na Ukraine.

Mamlaka ya Ukraine inachukulia Belarus kuwa moja ya wahusika katika mzozo huo, kwani wanajeshi wa Russia walitumia eneo lake kuivamia Ukraine.

**MAREKANI YATOA MSAADA ZAIDI**

Marekani itatuma Ukraine kifurushi cha ziada cha silaha chenye thamani ya dola milioni 725 na msaada mwingine wa kijeshi.

Ikulu ya Marekani ilisema jana kuwa msaada huo utajumuisha washirika wa Ulaya, huku kukiwa na mashambulizi mapya ya makombora katika maeneo yote ya Ukraine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema katika taarifa yake juzi kwamba msaada huo unafuatia kutokana na mashambulizi ya hivi karibuni.

"Kufuatia mashambulizi ya kikatili ya makombora ya Russia dhidi ya raia wa Ukraine, na ushahidi unaoongezeka wa ukatili unaofanywa na vikosi vya Russia". Alisema.

Kifurushi kipya zaidi cha kijeshi cha Marekani kinajumuisha makombora ya HIMARS na kuleta jumla ya msaada wa kijeshi wa Marekani kwa Ukraine hadi dola bilioni 18.3 tangu kuanza kwa utawala wa Joe Biden, Idara ya Ulinzi ilisema katika taarifa yake.

Marekani imetuma HIMARS 20 kwa Ukraine na imeahidi 18 zaidi ambazo zitawasilishwa katika miaka ijayo.

HIMARS imethibitika kuwa silaha muhimu ambayo imeboresha uwezo wa Ukraine kushambulia maghala ya risasi, madaraja na malengo mengine muhimu ambayo yanapunguza uwezo wa Russia kurudisha nyuma wanajeshi.

**BBC**

## Idadi ya waliofariki mgodini yapanda

**ANKARA,** UTURUKI

MAOFISA nchini Uturuki wamesema Idadi ya watu waliokufa kutokana na mlipuko katika mgodi wa Makaa ya mawe Kaskazini mwa nchi hiyo, imepanda na kufikia watu 40.

Shughuli za uokoaji zinaendelea huku moto ukiendelea kuwaka katika mgodi huo.

Wakati wa tukio hilo majira ya jioni, kulikuwa na wafanyakazi 110 waliokuwa ndani ya mgodi huo wa TTK Amasra Muessese Mudurlugu unaomilikiwa na serikali.

Waziri wa Nishati, Fatih Durmaz, alisema Juhudi zinaendelea za kuwafikia watu wengine 15 akiongeza kuwa wengi wamekwama katika eneo kunakowaka moto.

Waziri Durmaz alisema moto sio mkubwa sana lakini ni lazima uzimwe pamoja na gesi ya Kaboni iliyo na sumu kabla ya waokoaji kuendelea na operesheni yao.

Rais wa Uturuki, Tayyip Erdogan anatarajiwa kufika katika eneo la ajali. **DW**

## Watu 12 wauwawa DRC

**KINSHASA,** DRC

WATU wanaodaiwa kuwa wanamgambo wamewaua raia 12 kwa kuwakata kata kwa mapanga katika kijiji kimoja Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Tukio hilo limetokea katika eneo ambalo kwa miaka mingi limekuwa likikumbwa na machafuko kutoka kwa makundi yaliyojihami kwa silaha.

Akizungumza na shirika la habari la AFP, kiongozi wa shirika moja la kiraia katika eneo hilo, Gustave Kakani alisema watu hao, walikivamia kijiji cha Masome jimboni Ituri juzi asubuhi na kufanya uovu huo, wanawake na wanaume waliuwawa kwa kukatwa mapanga.

Baadhi ya miili ilipatikana ikiwa imekatwa viungo huku baadhi ikiwa imefungwa mikono.

Kakani alisema wahanga walipitia mateso mabaya kabla ya kuuwawa.

Hadi jana hakuna kundi lolote lililokiri kuhusika na shambulio hilo.

Kundi la waasi wa ADF ndilo kundi hatari zaidi kati ya vikundi zaidi ya 120 vya wanamgambo yanayolihangaisha eneo la Mashariki mwa Congo. **DW**

## MAKALA

# ANAISHI JAPO ALIFARIKI DUNIA



Na Magabilo Masambu

Mwanamuziki wa miondoko ya Reggae kutoka Afrika Kusini, Philipo Dube, maarufu kama Lucky Dube, katika moja ya albamu zake alikuwa na wimbo unaitwa "Rasta Never die" akiwa na maana kwamba rasta hawezi kufa.

Baada ya kifo chake, wako waliokuwa wakikejeli kwamba mbona alisema 'Rasta never die' na amekufa? Wako pia ambao hawakuwa wanaelewa maana ya kibao hicho. Lakini alichomaanisha Lucky Dube ni kwamba unaweza kufariki kimwili lakini mawazo na fikra zako zikaendelea kuishi kizazi hadi kizazi. Ndivyo ilivyotokea kwa waimbaji wengi wenye fikra na maono ya mbali. Nyimbo zao kila wakati ukizisikiliza utadhani wanasema sasa kumbe ni maneno yaliyoimbwa miaka mingi iliyopita.

Jambo hili ndivyo lilivyo hata kwa mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Ni miaka 23 sasa toka ameaga dunia, lakini ukisikiliza na kusoma maandiko yake unaona kama anaishi mpaka leo. Viongozi wa kariba yake duniani, huwa hawazaliwi mara kwa mara. Ni nadra sana kiongozi mwenye kujua kesho panaweza kutokea nini, ama anaonyeshwa akiwa kwenye ndoto au anayo maono ambayo yaweza kuwa ya kimungu.

"Katika tamko la 1967 la Elimu ya Kujitegemea, tulisema shule za sekondari zisiwe tu ni mahali pa kutayarisha vijana kuingia chuo kikuu au vyuo vingine vya elimu ya juu, bali zitayarishe vijana kwa kazi ya maendeleo ya taifa" (J.K Nyerere, Elimu ya Kujitegemea Baada ya mwaka 1967).

Maneno hayo Mwalimu aliyatamka miaka mingi iliyopita, lakini leo tunaweza kuwa mashahidi juu ya mfumo wetu wa elimu. Baada ya juhudi za muda mrefu za kujenga elimu ya kujitegemea kushindikana, tunaona kutatua tatizo la elimu ni kupanua elimu ya sekondari ili kuwaandaa vijana wengi kwenda katika elimu ya chuo kikuu au vyuo vingine vya juu.

Vyuo vikuu pia tukapanua ili wengi wapate digrii na kadhalika. Ni jambo jema, lakini tahadhari na mipango gani inachukuliwa ili kuhakikisha matokeo ya mwisho ya wanafunzi wengi wanaomaliza elimu ya juu watakavyokuwa baada ya kuhitimu kwa maana ya wapi watakwenda. Tungalikuwa na viwanda vingi wengine wangelifanya kazi za vibarua, lakini viwanda vingi alivyoacha Mwalimu vilikufa kwa hiyo jambo pekee lililobaki kama kimbilio la vijana hao ni kwenye kilimo.

Elimu ya Kujitegemea ilijikita zaidi katika kilimo tukawa na kauli mbalimbali kama kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kwanza lakini nadhani mipango yetu haikujikita zaidi kuweka mifumo wezeshi katika eneo la kilimo ili kuwafanya Watanzania wengi wawe na utaalamu wa kulima kitaalamu. Sasa hivi karibu shule zote zilizokuwa zinafundisha somo la kilimo zimekufa, zimebaki chache tukilinganisha na mahitaji ya Watanzania ambao ni kundi kubwa linalojiajiri kwenye kilimo.

Mwalimu alianzisha vyuo vya kilimo kwa lengo la kuzalisha wataalamu wa kilimo na wataalamu wa kwanza kabisa, ilikuwa kuzalisha walimu wengi wa somo la kilimo lakini leo hali ikoje katika shule zetu? Walimu wa kilimo hawapo. Lakini tunaambiwa zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wamejiajiri kwenye kilimo. Sasa watalimaje wakati elimu ya kilimo hawana?

Jambo la pili, Mwalimu alikemea sana kuhusu kuyatumia madaraka kujitajirisha ndiyo maana aliweka miiko ya uongozi katika Azimio la Arusha ambalo kwa kweli lilipingwa sana na baadaye likatupwa. Lakini leo miaka 23 hayupo kila mtu kwenye jamii pamoja na baadhi ya viongozi wetu, tunao mtazamo wa kwamba ukichaguliwa kuwa kiongozi tu tayari umepata ulaji.

Watu wanakupongeza kwa kuchaguliwa au kuteuliwa si kwa sababu unakwenda kuwatumikia bali ni kwa sababu wanaamini sasa utapata maisha mazuri sana na ikiwa utatoka madarakani huna mali, watakushangaa na kukuona mtu wa ajabu sana. Je, kwa mtindo huu tutapiga hatua za kimaendeleo kama taifa?

Katika maeneo mengine tunaweza kujisifu kidogo, hata kama si kwa kiasi kikubwa sana angalau tumejitahidi hasa katika eneo la ukabila kwani hatujafarakana kwa misingi ya ukabila. Ukanda na urafiki pia hatujisifu sana, vipo vidalili ambavyo nafikiri kutokana na ubinafsi wa binadamu huwa haviondoki kabisa lakini juhudi zinahitajika kuendele kupiga vita mambo ya ukabila, ukanda na urafiki katika ama kuteuawana au kuchaguana.

Udini vilevile bado naamini tuko vizuri kama taifa. Hatujawahi kutofautiana kwa misingi ya dini zetu pamoja na kwamba tunazo dini tofauti tofauti tunashirikiana shughuli ya Mkristo ni ya Mwislam na ya Mwislamu ni ya Mkristo. Haya yanatufanya tumuone Baba wa Taifa kwamba anaishi wakati alishafariki dunia.

Vilevile Muungano wetu tumeendelea kuudumisha. Ni jambo jema kabisa kwa sababu ni wapumbavu tu ndio wanaweza kuvunja umoja wakati wenye akili huko duniani wanaungana kutukabili sisi wanyonge. Kama tunaona katika Muungano, ziko changamoto, hizo tuzizungumze lakini tusitangulize kuuvunja. Ukweli ni kwamba wakati mwingine tunauona hauna maana kwa sababu tumo ndani yake, sawasawa na ambavyo umuhimu wa mtu hauonekani mpaka aondoke. Ukivunjika tutaona shuruba zake tuendelee kumuenzi mwalimu kwa kuudumisha Muungano wetu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Utata sababu wimbo 'Bomoa tutajenga Kesho' kupigwa marufuku kuimbwa RTD



Na Adam Fungamwango

MOJA ya matukio ambayo yalishangaza mashabiki wa muziki wa dansi nchini katikati ya miaka ya 1980 ni kusitishwa kupigwa kwa wimbo uliokuwa maarufu na kupendwa mno 'Bomoa Tutajenga Kesho.'

Kwa muda mfupi tu baada ya kurekodiwa, wimbo huo 'ukahiti' watoto wa kisasa wanasema, hata watoto wadogo mtaani wakawa wanauimba. Ulijulikana zaidi kuliko hata bendi yenyewe iliopiga ambayo inaitwa Orchestra Mambo Bado.

Mtunzi wa wimbo huo ni mwanamuziki maarufu Afrika Mashariki na Kati, Tshimanga Kalala Asossa. Wimbo huo una mashairi yafuatayo;-

"Bomoa eee Bomoa eee Bomoa mama tutajenga kesho imaa, tujajenga kesho imaa oo

Imaao enyi watoto wazuri wote, njoni tucheze leo bomoa

O betu bayai yoyoyo bomoa

Bomoa eee Bomoa eee Bomoa mama tutajenga kesho imaa, Tujajenga kesho imaa oo

Kumbe njoni wote tucheze bomoa, kumbe njoni wote tucheze bomoa."

Ukisoma mashairi haya, utagundua kuwa wala haukuwa na maneno mengi sana au mashairi marefu. Badala yake ulivyotengenezwa kwa mpangilio wa maneno yanavyotakwa, sauti za waimbaji na vyombo vilivyopangilia, ilikuwa inatoa raha kuusikiliza.

Msomaji yoyote wa kizazi cha sasa anaweza kushangaa kwa sababu hauna maneno yoyote yenye ukakasi kama nyimbo nyingi za kisasa za bongo fleva ambazo huwezi kuzisikiliza mbele ya watu unaowaheshimu.

Kwa kawaida, zamani bendi kabla ya kwenda kurekodi Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), zilipeleka mashairi ya nyimbo zote zinazohitaji kurekodiwa, halafu kuna Kamati ya Maadili ambayo inakaa na kupitia maudhui, na mpangilio wa maneno, lugha na hata tafsiri ya wimbo wenyewe, una manufaa gani kwa jamii.

Vigezo vikitimia wimbo unarekodiwa, lakini kama kuna kasoro mashairi yanarudishwa kwa bendi husika ili kurekebisha, wakipewa na muongozo wa maneno ambayo yanapaswa kutumia kama wataona yanafaa au kuingia kwenye mapigo ya wimbo wenyewe. Baada ya hapo wimbo unakubaliwa kurekodiwa.

Cha kushashangaza ni kwamba wimbo huu ulitimiza vigezo vyote. Ulipita kwenye tanuru la moto hadi wakaupitisha kurekodiwa. Lakini baada ya kupata umaarufu wa ghafla, ukasikitishwa kupigwa RTD na kushangaza mashabiki wengi sana ambao walikuwa wakiuomba kila siku kwenye vipindi vya salamu, ugua pole, pole kwa kazi na vingine. Na kwa sababu wakati huo redio ilikuwa moja tu, haukusikika tena, ikawa majonzi na huzuni kwa mashabiki.

Kwa mujibu wa mmoja wa wanamuziki wa bendi hiyo, John Kitime ni kwamba hata wao kwenye ukumbi sasa walianza kuupiga kwa 'wizi wizi' kwani aliogopa. Hadi leo hii ninavyoandika kwenye safu hii hakuna sababu halisi ya kwa nini wimbo huo ulipigwa marufuku.

hakuna mtu yeyote aliyejitokeza akasema anaupiga marufuku wimbo huo na kwa sababu gani. Badala yake sasa mitaani kama kawaida, pamoja na kwamba hakukuwa na mitandao ya kijamii, vijiwe vilikuwapo, kila mtu alikuwa anaongea lake.

Wengi walisema baada ya wimbo huo kutoka na kuwa maarufu, huko Dodoma baahi ya watu walikuwa wakibomoa barabara zilizojengwa na wakoloni wakisema watajenga za kwao kesho kama wimbo huo unavyoimbwa.

Wengine walisema ulipigwa marufuku kwa sababu watu walianza tabia mbaya ya kutumia ovyo walichokipata mfano pesa kwa kulewa wakidai kesho zitapatikana zingine, hivyo kushawishi wengine kuwa tabia ya kupanya pesa bila kuweka akiba.

Maneno na uvumi ulikuwa mwingi mno, lakini Kitime mmoja waliorekodi wimbo huo anasema hata wao walishtukia tu katazo hilo kwenye gazeti.

"Siku moja tukasoma kwenye gazeti likidai Umoja wa Vijana wa Dar es Salaam umepiga marufuku mambo kadhaa, kwanza wanamuziki, watu maarufu na wasanii kujiita 'aka' zilizokuwa za lugha za kigeni, mwanamieleka mmoja alikuwa anajiita Power Savimbi akambiwa asitumie tena jina hilo, ikawa marufuku kusema shule za vidudu, ila ziitwe chekechea, wacheza shoo walipigwa marufuku, na wimbo huo pia ulipigwa marufuku, ikawa hausikiki tena redioni japo bendi tuliendelea kuupiga kwa wizi. Mpaka leo sijaweza kujua hasa kwa nini wimbo huo ulipigwa marufuku."

Anasema Kitime ambaye alipiga gitaa ya rhythm kwenye wimbo huo.

Akizungumzia kisa cha Asossa kuanzisha bendi hiyo ambaye haikudumu sana pia kutunga wimbo huo anasema walitukana na mwanamuziki hiyo kwenye studio za TFC, Mikocheni akawaambia kuwa ana mpango wa kuanziasha bendi.

Ilianzishwa na makao makuu yaliyokuwa Mabibo, nyuma ya Ubungo Maziwa na kulikuwa na mfanyabiashara mmoja aliyekuwa anataka kufungua baa na mgahawa, hivyo mpango uliandaliwa bendi, baa na mgahawa vizinduliwe siku moja.

Anasema getini kulikuwa na geti kubwa la chuma kiasi kwamba hata baa yenyewe ikaitwa Lango la Chuma.

"Siku chache kabla ya ufunguzi mfanyabiashara yule alipita kuangalia mazoezi na mmoja ya wanamuziki akamtania kuwa tayari kulikuwa na ufa kwenye geti kwa sababu ya mazoezi tu ya bendi, hivyo siku ya uzinduzi ukuta utabomoka kwa kujaa watu. Jibu la yule mfanyabiashara lilikuwa 'bomoa tutajenga kesho.'"

Wanamuziki wakalipenda lile neno, na Asossa akatunga wimbo huo, hata staili ya uchezaji wa shoo ikaitwa Bomoa. Wimbo uliporekodiwa ukatokea kupendwa sana na kuwa nembo ya bendi," anasema Kitime.

Baada ya miaka kadhaa ulianza kupigwa tena. Hata hivyo kwa sasa wimbo huo unapigwa kama kawaida kwenye vipindi mbalimbali vya muziki wa zamani.

**Tuma meseji 0716 350534.**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.
Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi Imevunjika-1

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**

"Umeweka doa kubwa sana kwenye maisha yangu ambalo halitoweza kuzibika hili la kuniacha na kunikimbia siku ya harusi. Siamini kama mimi na wewe huu ndiyo mwisho wetu Vayajo, kwa jinsi nilivyokuwa nimekuweka kwenye moyo wangu.

Ulitaka nifanye nini? Nilijitolea kwa hali na mali, nikakupa furaha na kuwa na amani. Haya ndiyo malipo yangu Vayajo? Nini kilichotugombanisha mimi na wewe ni nini? Ndugu zangu wametoka mikoa mbalimbali wamekuja huku, wananiuliza Vayajo yupo wapi? Sina la kuwajibu, nimebaki na kilio kisichokuwa na mbembelezaji.

Vayajo, kwa nini umefanya hivi? Umenipa pigo ambalo sitolisahau maishani. Kila mtu kwenye harusi ananiangalia mimi, wengine wananionea huruma, wengine wananicheka naona aibu."

"Mama mkubwa ametoka Morogoro kutaka kumuona Vayajo, Mama Kamwaya ametoka Tanga kuja kukuona, Baba mdogo kutoka Sumbawanga naye amekuja kwenye harusi hii kwa ajili ya kumuona bibi harusi alivyopendeza, alivyovaa shela ya harusi. Bibi hakuja huku, amebaki nyumbani kutokana na umri wake mkubwa, naye anasubiria turudi nyumbani amuone Vayajo.

Upepo unavuma, gari inazidi kuongeza mwendo kurudi nyumbani, moyo wangu unaumia kwa simanzi. Watu walitupungia mikono Kibaha kutuaga, lakini wengine wanatusubiri Dar es Salaam. Sijui nitaweka wapi uso wangu."

"Jioni ilifika bibi harusi hayupo, usiku umeingia Vayajo haonekani, kesho itakuja, mpenzi ametoweka, kazi iliyobaki kwa ndugu zangu ni kukaa na mimi, kunizunguka ili nisije nikachukua maamuzi mabaya ya kujinyonga.

Nikikumbuka siku ya kwanza nilipokutana naye ilikuwa ya furaha sana, tumeishi kwa mapenzi ya hali ya juu, hatujawahi kugombana. Hujawahi kunikosea au kukukosea, umenyeshwa dawa gani hadi kunifanya hivi?"

"Kabla ya kifo changu nitawaambia ndugu uhudhurie msiba wangu, wasikufukuze ushuhudie maiti yangu inavyolia machozi kwa ajili yako Vayajo. Labda maiti yangu inaweza kukupa ishara itakayoonyesha kuwa mimi nakupenda kuliko kitu kingine chochote kuliko hivi nilivyo hai. Inawezekana mdomo na vitendo vyangu bado havijakuaminisha kuwa ni kweli nakupenda. Kupenda kwangu kumekuwa sumu kubwa kwenye maisha yangu. Mbona zamani hukuwa hivyo? Umepatwa na nini mpenzi?"




**"Bwana kapata bibi na bibi kapata bwana, kimasomaso mwanangu msimuone, mwenye jicho la adui." Nyimbo ziliendelea kukolea.**

"Kwa hili lililotokea nadhani sitopenda tena mwanamke mwingine. Kwa sababu kama Vayajo alinipenda, nilimpenda tukapendana lakini amegeuka hivi kunidhalilisha mbele ya umati wa watu, nitawezaje kumuamini mwingine?

Nalia muda wa miaka mitatu ambayo tumekuwa wote nimeupoteza bure, nalia gharama zote mimi na ndugu zangu tulizoingia kufanikisha sherehe hii. Watu wamejitolea gharama na muda, lakini wameishia kupata aibu, mshangao na huzuni."

Kilikuwa ni kilio kizito. Kilio cha huzuni kutoka kwa Jerry. Bwana harusi aliyetoka Dar es Salaam na ujumbe wake kwenda mkoani Pwani kijiji cha Msangani, kilometa saba Kaskazini mwa eneo la Kibaha kwa Mathias.

Msafara ulifika, watu wote waliteremka kwenye magari, akinamama wakiimba na kucheza nyimbo mbalimbali zingine zikiwa na maneno kuwa wanamtaka mke wao.

Alikuwa akiongea maneno hayo kwa sauti akilia na kuomboleza akiwa kwenye gari huku macho yake mbele kama yakiwa yanamuona Vayajo. Maneno hayo alikuwa akimwambia Vayajo asiyekuwepo, bali ni taswira ambayo alikuwa ameitengeneza kichwani mwake akiwa kama amechanganyikiwa.

Kila kitu kilienda kama kilivyopangwa, bwana harusi alijiandaa kwa ajili ya kufungishwa ndoa. Wapambe sasa walikwenda kwenye chumba cha bibi harusi ambaye mara ya mwisho alionekana saluni akipambwa na akapambika.

Katika hali isiyotarajiwa na kushangaza, bi harusi hakuwepo chumbani. Aliyekuwa amekaa naye chumbani alisema alitoka kidogo kwenda msalani na aliporudi hakumkuta lakini hakuwa na wasiwasi, inawezekana ametoka mara moja kwenda uani.

Robo saa ilipita bila kuonekana. Hali ya wasiwasi ikaanza kutawala chumbani humo. Wakaitwa kina shangazi, mama mzazi na wengine. Nao wakajionea kilichoonekana. Wakashika vichwa.

"Yuko wapi mwana huyu, mbona anataka kunitia aibu mimi?" Mama mzazi alisema huku akiwa ameshika kichwa, akitafuta chumba hiki na kile.

Kila dakika zilivyozidi kwenda mbele ndivyo hali ilivyozidi kuwa mbaya chumbani. Huko nje ngoma na shamrashamra ziliendelea kama kawaida.

"Bwana kapata bibi na bibi kapata bwana, kimasomaso mwanangu msimuone, mwenye jicho la adui." Nyimbo ziliendelea kukolea.

"Wangejua hawa!" Mmoja aliyekuwa chumbani mwa bi harusi alijisemea, maana kwa ile hali alionekana na wanapiga kelele tu.

Baada ya akili zao kuamini kile kilichotokea, wanandugu wakaanza kutoka nje mmoja mmoja. Waliobaki ndani walikuwa wanalia, lakini si kwa sauti. Ni kwa sababu suala lile kwao ilikuwa ni kama aibu kubwa.

Hata wale waliotoka nyuso zao hazikuwa na nuru. Kuna waliobaki nje wenye akili ya kujiongeza wakawa kama wamehisi jambo.

Mzee mmoja ambaye baada ya kuambiwa kilichotokea, hakutaka watu wahamanike au kuleta mhaho na taharuki, alikwenda kwa wapiga ngoma na kuwataka wasimamishe kwanza.

"Jamani eee, samahanini kwanza, tumeona kwamba badala ya kuendelea na ratiba nyingine kwanza kipakuliwe chakula watu wale, maana wengine wametoka mbali Dar es Salaam tangu asubuhi hawajala, kwa hiyo msosi upakuliwe watu wale, na ratiba zingine zitaendalea kama zilivyopangwa."

Nia ya mzee yule ni kwamba watu wale chakula kilichopikwa kwanza, halafu kama baadaye itatangazwa habari hiyo mbaya, tayari kila mtu atakuwa ameshakula, tofauti na kile kilichopo sasa kama kitatangazwa, basi kuna watu hata kula hawatokumbuka tena kwa sababu halikuwa suala la kawaida.

Kwa sababu ni suala la chakula hakuna aliyehoji, na ni watu wachache sana waliofahamu tukio la kutoweka kwa bi harusi.

Sehemu kama hizo umbea haukosekani. Kuna baadhi wakaanza kuvujisha habari kabla hazijatamkwa rasmi. Wengi hawakuamini na ilionekana ni kama ni moja ya habari za mzaha tu ili kusukumizia chakula na vinywaji tu.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# LISU, SINACH HAPATOSHI DIAMOND JUBILEE

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili Sinach Joseph Egbu toka Nigeria, kwa kushirikiana na John Lisu wataongoza jukwaa la Festival of Praise katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam leo.

Lisu ambaye ni muandaaji wa tamasha hilo, ameliambia gazeti hili kuwa Sinach atafanikisha ujumbe wa neno la Mungu kwa Watanzania kupitia tungo zake na waimbaji wengine wa hapa nchini.

"Nitashirikiana naye, huku yeye Sinach akipanda jukwaani na wimbo wake uliokamata anga la muziki wa Injili duniani wa 'Way Maker' uliotazamwa na mashabiki zaidi ya milioni 200," amesema Lisu

Amewataja waimbaji watakaomsindikiza mwimbaji huyo ni Christina Shusho, Ambwene Mwasongwe, Pasta EPA, Kwaya ya Kanisa la Moravian, Ruach Worship Team kutoka Kenya na Kwaya ya Gospel Winners.

# WASANII WA KIKE WAPIGWA MSASA

**Na Halfani Chusi**

Kipindi cha Corona kilisababisha kupotea kwa wasanii wengi wa kike ambao kimsingi ndio chachu ya kukua kwa sanaa nchini walishindwa kufanya kazi.

Wasanii waliokuwa kwenye lebo walifukuzwa kwa sababu walikuwa hawaingizi faida na wengine walikosa kazi za kujiingizia kipato.

Kutokana na kuwapo kwa vitendo hivyo mtandao wa wasanii wanawake Tanzania, uliamua kutoa elimu kwa wasanii wa kike namna bora ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Mwenyekiti wa jukwaa la wanawake Tanzania Aginesi Lukanga, aliliambia Nipashe kuwa, kupitia mateso waliyopata wasanii wanawake katika kipindi cha Corona walibaini mambo mengi na hivyo walianza kutoa elimu na namna ya kuwakomboa.

"Kwa kutumia kauli mbiu yetu ya 'tuseme tusichoke' tuliendesha mafunzo kwa wasanii wanawake lengo lilikuwa ni kuwajengea uwezo ili siku nyingine linapotokea gonjwa la mlipuko tofauti na Corona waweze kuendelea kufanya kazi zao na kujipatia kipato"



## ZISIKUPITE

### MADRID HAIMFIKIRII MBAPPE
KLABU ya Real Madrid bado haijafikiria kutoa ofa nyingine kwa ajili ya kumsajili fowadi wa Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 23, Kylian Mbappe. ***(ESPN)***

### MARIN ATAKIWA PSG
KLABU ya PSG inawania kumsajili mlinzi wa kati wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 20, Rafa Marin. ***(Marca)***

### LUKAKU, INTER KIMEELEWEKA
KLABU ya Inter Milan inataka kumsajili Romelu Lukaku kwa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Ubelgiji anacheza hapo kwa mkopo akitokea Chelsea. ***(Calciomercato)***

### MINA KUTUA EVERTON
KLABU ya Inter Milan pia inamwania mlinzi wa kati wa Everton na Timu ya Taifa ya Colombia mwenye umri wa miaka 28, Yerry Mina. ***(Calciomercato)***

### COSTA AKARIBIA UNITED
KLABU ya Manchester United ina nafasi nzuri zaidi ya kumsajili golikipa wa Porto mwenye umri wa miaka 23, Diego Costa. ***(Diario de Noticias, via TeamTalk)***

### DALOT MAMBO MAZURI
MANCHESTER United itamwongezea mkataba, Diogo Dalot ili kuzuia nia ya Barcelona inayomtaka mchezaji huyo mwenye umri wamiaka 23 raia wa Ureno. ***(ESPN, via Mirror)***

### GUIMARAES KUZEEKEA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inataka kumpa mkataba wa muda mrefu kiungo Timu ya Taifa ya Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 24, kabla ya mwishoni mwa msimu huu. ***(90min)***

### MUDRYK KUIKAMUA ARSENAL
ARSENAL wanaweza kutakiwa kulipa zaidi ili kumsajili winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21 Januari, kama klabu yake ya Shakhtar Donestk itasonga mbele kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Football.London)***

### CONTE, SPURS KUTETA
KLABU ya Tottenham inapanga kufungua mazungumzo na kocha wake, Antonio Conte, mwezi ujao. Mkataba wa Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 53 utamamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### JOAO KUONDOKA ATLETICO
FOWADI wa Atletico Madrid mwenye umri wa miaka 22 raia wa Ureno, Joao Felix, anataka kuondoka klabuni hapo Januari kutokana na mahusiano mabaya na kocha, Diego Simeone. ***(A Bola)***

### DAVIES ANUKIA MADRID
REAL Madrid inafikiria kumsajili mlinzi wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 21. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP HOFU TELE AKIWAKABILI CITY

## Amtaja Haaland ndiye anamhofia zaidi huku akikiri timu yake haiko...

**LONDON, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekiri Erling Haaland ndio "mshambulizi bora zaidi duniani" kuelekea katika mchezo wao wa leo dhidi ya Manchester City utakaochezwa kwenye Uwanja wa Anfield.

Haaland tangu atue katika Ligi Kuu England amefunga mabao 15 ya kushangaza katika mechi zake tisa za kwanza, na pia ametawala katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufikisha jumla ya magoli 20 hadi sasa msimu huu.

Raia huyo wa Norway alipumzishwa wakati City ilipotoka suluhu dhidi ya Copenhagen katikati ya wiki, lakini leo anatarajia kuongoza mashambulizi dhidi ya Liverpool kwenye mchezo huo.

Wekundu hao kwa upande wao, wamekuwa na mwanzo wa taratibu, huku wakikabiliwa na wachezaji wengi majeruhi.

Liverpool wameshinda mechi mbili pekee kati ya nane za Ligi Kuu England, na wanawafuata City wakiwa wamepitwa pointi 13, kitu kinachomfanya Klopp kukiri klabu hiyo ipo nje ya mbio za ubingwa msimu huu.

Liverpool walipata ushindi mnono Jumatano usiku wakati wakishinda mabao 7-1 dhidi ya Rangers katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Klopp alikuwa anajua sana tishio ambalo Haaland atalileta leo wakati akizungumza na vyombo vya habari.

"Labda ni mshambuliaji bora zaidi duniani kwa hiyo lazima tuhakikishe hapati mipira mingi," alisema Klopp raia wa Ujerumani wakati alipoulizwa ni vipi timu yake itapambana na tishio la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Hilo ndilo tutajaribu. Dhidi ya City ukimwacha Haaland na wachezaji wengi wana uwezo wa kufunga, hivyo mambo hayatakuwa rahisi.

"Ana mchanganyiko mzuri kimwili na kiufundi. Anajua mahali ambapo anaweza kufunga kiurahisi.

"Ujuzi wake wa kumalizia ni wa kipekee, lakini anasonga kwa akili sana. Unaweza kutumia kasi tu ikiwa utaitumia kwa njia nzuri."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS.374,

MECHI KALI

REAL MADRID
VERSUS
BARCELONA

1 | 2.23
X | 3.54
2 | 2.94

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# N'GOLO KUKOSA KOMBE LA DUNIA



**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, anatarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu kutokana na jeraha la misuli ya paja na hivyo kumfanya akose kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadae mwezi ujao nchini Qatar.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameichezea Chelsea mechi mbili pekee na hajacheza tangu mechi ya pili ya Ligi Kuu England msimu huu, ambayo walitoka sare ya mabao 2-2 na Tottenham Hotspur.

Ripoti kutoka Ufaransa zilidokeza Alhamisi asubuhi, Kante aliumia msuli wa paja na Kocha, Graham Potter, alifichua katika mkutano wake na waandishi wa habari alikuwa na shida katika kupona kwake na alitakiwa kuonana na mtaalamu.

Lakini ripoti mpya kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, Kante huenda akakaa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu - na kumfanya kukosa michuano ya Kombe la Dunia, ambayo itaanza Novemba 20, mwaka huu.

Mfaransa huyo, ambaye ni mshindi mara mbili wa Ligi Kuu England akiwa na Leicester na Chelsea, mkataba wake unamalizika Stamford Bridge msimu ujao wa joto na inasemekana anataka kuongezewa.

Hata hivyo, Kante amekuwa na majeraha kadhaa ya misuli katika misimu michache iliyopita, na amecheza mechi chache tangu msimu wa 2019/20.

Potter alikiri kwa vyombo vya habari kwamba, Kante kwa sasa anakabiliwa na wakati mgumu, lakini hakutaka kufafanua zaidi ni lini Kante anaweza kurejea Chelsea.


# Neymar hatarini kufungwa

**BARCELONA, Hispania**

SHIRIKA la Uwekezaji la Brazil (DIS), linataka Neymar afungwe miaka mitano atakapofikishwa mahakamani wiki ijayo kujibu mashitaka ya ulaghai na ufisadi yanayohusiana na uhamisho wake wa kwenda Barcelona kutoka Santos mwaka 2013.

DIS, ambalo lilikuwa linamiliki asilimia 40 ya haki ya mshambuliaji huyo wa Brazil linadai lilipata hasara baada ya kukosa ada ya uhamisho wake unaokadiriwa ulikuwa wa chini.

Neymar mwenye umri wa miaka 30, amekanusha madai hayo, lakini alipoteza rufaa aliyowasilisha katika Mahakama Kuu ya Hispania mwaka 2017, na kufanya kesi hiyo kufikishwa mbele ya waendesha mashitaka wa nchi hiyo.



Mchezaji huyo wa Paris St-Germain atalazimika kufika mahakamani siku ya kuanza kwa kesi hiyo Barcelona Jumatatu ijayo, lakini haijabainika kama ataamrishwa kusalia jijini humo hadi kesi yote itakaposikilizwa na kuamuliwa ndani ya wiki mbili.

Washitakiwa wengine ni wazazi wa Neymar, klabu hizo mbili, mabosi wa zamani wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu na Sandro Rosell, na Rais wa zamani wa Santos, Odilio Rodrigues.

Rosell pia hapo awali alikanusha makosa yoyote. Katika taarifa, Baker McKenzie, wakili anayewakilisha familia ya Neymar, alidai mahakama za Hispania "hazina mamlaka ya kushitaki familia ya Neymar na kampuni yao ya N&N" kwa sababu vitendo hivyo vilifanywa na raia wa Brazil nje ya eneo la Hispania.

,935,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/10/22 | 20:00 | Cadiz CF vs Betis | 2.85 | 3.25 | 2.43 |
| 02. 19/10/22 | 20:00 | Valladolid vs Celta Vigo | 2.47 | 3.19 | 2.85 |
| 03. 19/10/22 | 20:00 | AIK Football vs BK Hacken | 2.39 | 3.40 | 2.58 |
| 04. 19/10/22 | 21:30 | Bournemouth vs Southampton | 2.72 | 3.27 | 2.46 |
| 05. 19/10/22 | 21:30 | FC Luzern vs St. Gallen | 2.50 | 3.55 | 2.55 |
| 06. 19/10/22 | 21:45 | Wigan vs Middlesbrough | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 07. 19/10/22 | 21:45 | Mechelen vs Standard Liege | 2.54 | 3.39 | 2.59 |
| 08. 19/10/22 | 22:00 | Millwall vs Watford | 2.71 | 3.20 | 2.51 |
| 09. 19/10/22 | 22:15 | Manchester Utd vs Tottenham | 2.23 | 3.42 | 2.94 |
| 10. 20/10/22 | 20:00 | Almeria vs Girona | 2.35 | 3.20 | 3.00 |
| 11. 20/10/22 | 20:00 | Degerfors vs IFK Goteborg | 2.73 | 3.32 | 2.31 |
| 12. 20/10/22 | 21:00 | Osasuna vs Espanyol | 2.22 | 3.20 | 3.25 |
| 13. 20/10/22 | 21:30 | Fulham vs Aston Villa | 2.77 | 3.22 | 2.45 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 16/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 1678 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 13:30 | 2820 | Inter vs Salernitana | 1.28 | 5.53 | 8.30 |
| 14:00 | 1321 | Dalkurd FF vs Ostersunds | 2.41 | 3.37 | 2.87 |
| 14:00 | 1830 | Motherwell vs Rangers | 7.35 | 4.77 | 1.37 |
| 14:00 | 5628 | Toulouse vs Angers | 1.83 | 3.73 | 3.83 |
| 15:00 | 4165 | Brondby vs Copenhagen | 2.84 | 3.39 | 2.33 |
| 15:00 | 4276 | Viborg FF vs Odense | 1.72 | 3.68 | 4.48 |
| 15:00 | 5557 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 16:00 | 1235 | Rennes vs Lyon | 2.32 | 3.50 | 2.80 |
| 16:00 | 1267 | Nantes vs Brest | 2.16 | 3.24 | 3.29 |
| 16:00 | 2712 | Southampton vs West Ham | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 16:00 | 2823 | Leeds vs Arsenal | 5.08 | 3.95 | 1.59 |
| 16:00 | 4151 | Troyes vs AC Ajaccio | 2.13 | 3.14 | 3.49 |
| 16:00 | 4265 | Manchester Utd vs Newcastle | 1.98 | 3.55 | 3.40 |
| 16:00 | 4440 | Aston Villa vs Chelsea | 4.25 | 3.61 | 1.76 |
| 16:00 | 4828 | Lazio vs Udinese | 2.15 | 3.46 | 3.07 |
| 16:00 | 5162 | AJ Auxerre vs Nice | 3.44 | 3.39 | 2.04 |
| 16:00 | 5286 | Spezia vs Cremonese | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 16:30 | 1616 | FC Koln vs Augsburg | 1.66 | 3.97 | 4.46 |
| 17:00 | 3328 | Aberdeen vs Hearts | 2.25 | 3.38 | 2.99 |
| 17:00 | 4652 | Basaksehir vs Istanbulspor | 1.42 | 4.47 | 6.76 |
| 17:00 | 5055 | KAA Gent vs Mechelen | 1.51 | 4.28 | 5.57 |
| 17:00 | 5243 | Shakhtar Donetsk vs Dynamo Kiev | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 17:15 | 1075 | Real Madrid vs Barcelona | 2.23 | 3.54 | 2.94 |
| 17:30 | 2130 | Servette Geneva vs FC Basel | 2.25 | 3.59 | 2.84 |
| 17:30 | 2275 | FC Zurich vs BSC Young Boys | 3.38 | 3.83 | 1.93 |
| 17:45 | 2938 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.45 | 3.43 | 2.63 |
| 18:00 | 1641 | PAS Giannina vs OFI Crete | 2.20 | 3.15 | 3.35 |
| 18:00 | 3359 | Austria Vienna vs RB Salzburg | 4.47 | 3.89 | 1.61 |
| 18:00 | 5835 | Valerenga vs Bodo Glimt | 2.73 | 3.57 | 2.33 |
| 18:05 | 4412 | Monaco vs Clermont Foot | 1.33 | 5.14 | 7.92 |
| 18:30 | 1527 | Liverpool vs Manchester City | 3.65 | 3.88 | 1.82 |
| 18:30 | 2080 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 2.92 | 3.37 | 2.27 |
| 18:30 | 5866 | Mjallby vs Hammarby | 3.90 | 3.56 | 1.78 |
| 19:00 | 2483 | Napoli vs Bologna | 1.24 | 5.73 | 9.87 |
| 19:00 | 3448 | Midtjylland vs Horsens | 1.50 | 4.27 | 5.76 |
| 19:30 | 2039 | Lamia vs Panathinaikos | 5.76 | 3.48 | 1.63 |
| 19:30 | 2594 | Malaga vs Lugo | 1.96 | 3.22 | 3.86 |
| 19:30 | 2784 | Gornik Zabrze vs Lech Poznan | 2.96 | 3.35 | 2.16 |
| 19:30 | 4686 | Espanyol vs Valladolid | 2.10 | 3.30 | 3.45 |
| 19:30 | 4942 | Anderlecht vs Brugge | 2.48 | 3.43 | 2.63 |
| 19:30 | 5846 | Partizan vs Cukaricki St | 1.48 | 4.10 | 5.47 |
| 20:00 | 1305 | CSKA Moscow vs Spartak Moscow | 2.20 | 3.47 | 2.97 |
| 20:00 | 2478 | Lillestrom vs Molde | 2.73 | 3.43 | 2.40 |
| 20:30 | 1409 | Asteras Tripolis vs Panetolikos | 1.84 | 3.34 | 4.29 |
| 20:30 | 4847 | Bayern Munchen vs SC Freiburg | 1.24 | 6.14 | 9.11 |
| 21:00 | 4956 | Ajax vs SBV Excelsior | 1.05 | 11.95 | 24.90 |
| 21:45 | 1634 | Verona vs AC Milan | 5.54 | 4.05 | 1.53 |
| 21:45 | 4891 | Paris St Germain vs Marseille | 1.40 | 4.79 | 6.63 |
| 22:00 | 1968 | Betis vs Almeria | 1.55 | 4.09 | 5.59 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MGUNDA AMTAJA KAPOMBE, AKPAN KATIKA MAPAMBANO

**Na Hadija Mngwai**

HUKU kikosi cha Simba leo kikitarajia kuwakaribisha Primeiro de Agosto kutoka Angola katika mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, amesema kukosekana kwa mabeki wake, Shomari Kapombe na Victor Akpan kunamchanganya.

Nyota hao wawili ni majeruhi ya muda mrefu na wameshindwa kuitumikia Simba tangu kuanza kwa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema anawaombea nyota wake hao afya zao ziimarike na kurejea katika majukumu yao kama ilivyotarajiwa.

Mgunda alisema kama mabeki hao wangekuwepo, timu yake ingekuwa imara zaidi na maana ya kikosi kipana ingeendelea kutawala.

"Nimewamisi wanangu Kapombe na Akpan, nawaombea ili wawe sawa warejee katika kikosi kwa ajili ya kuungana na wenzao katika mapambano haya ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa. Banda (Peter), yupo vizuri baada ya kuanza mazoezi ila Kapombe na Jimmyson (Mwanuke), bado wanaendelea na matibabu, lakini wakati wowote watajiunga na wenzao kuendeleza mapambano na kwa upande wa Akpan maumivu yake yamepungua kwa kiasi kikubwa sasa hivi anaendelea vizuri hivyo kadri anavyoendelea kupata matibabu ndivyo anavyokaa sawa. Kurudi kwao kikosini kutasaidia licha ya Simba kuwa na wachezaji wengi," alisema Mngunda.

Kuelekea mchezo wa le, kocha huyo alisema wamejiandaa kusaka ushindi huku akisisitiza bado kazi haijamalizika.

"Tunaenda kupambana kusaka ushindi, mchezo bado haujaisha, hadi uishe ndio tutajua mwelekeo wetu, mpira una maajabu na unaweza kupa matokeo usiyoyatarajia," Mgunda aliongeza.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Oppa Clement (katikati) akifunga bao katika mechi ya kirafiki kujiandaa na fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake dhidi ya wenyeji Ceasiaa Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa Samora mkoani Iringa juzi. Simba Queens ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Serengeti Girls

INATOKA UK. 24

Ufaransa.

Mechi nyingine iliyocheza mapema jana ilishuhudiwa Colombia wakiichapa China mabao 2-0.

**Wakati huo huo,** Serengeti Boys imemaliza katika nafasi ya tatu katika mashindano ya CECAFA (U-17), baada ya kuwafunga Uganda penalti 4-1, timu hizo zilimalizika dakika 90, zikitoka sare ya bao 1-1.

Fainali ya mashindano hayo yanayofanyika kwenye Uwanja wa Abebe Bikila, Ethiopia zilitarajiwa kuwakutanisha Somalia dhidi ya Sudan Kusini.

## Simba, Yanga, Azam kazini

INATOKA UK. 24

wa kwenye hatua ya makundi, lakini na sisi ni wazuri pia. Nimewaambia wacheze kwa ajili ya mashabiki," alisema Nabi.

Kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kuanzia saa 1:00 usiku, wenyeji Azam FC watakuwa na kibarua kizito cha kupindua matokeo, itakapocheza na timu ngumu ya Al Akhdar kutoka Libya.

Waarabu hao wataingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0, walioupata kwao Oktoba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Martyrs of February jijini Benghazi.

Kama wenyeji wanataka kusonga mbele na kuendelea kwenye michuano hiyo ya kimataifa ya CAF wanahitaji ushindi wa kuanzia mabao 4-0.

Mabingwa wa Kombe la FA, Kipanga yenyewe iko Tunisia kwenye Uwanja wa Olympique de Rades kuwakabili wenyeji Club Africain, katika mechi ya mkondo wa pili wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.

Mashindano ya ZFF, mchezo huo umesogo

Michezo
Jumapili Oktoba 16, 2022
Nipashe



Klopp hofu tele akiwakabili City
UKURASA 21




Straika wa Serengeti Girls, Aisha Mnuka (katikati), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Ufaransa katika mechi ya Kundi D ya fainali za Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Pandt Jawaharial Nehru, Goa nchini India jana. Serengeti Girls ilishinda mabao 2-0. **PICHA: TFF**

# Simba, Yanga, Azam kazini

## Kila timu yaahidi kusaka ushindi katika michuano hiyo ya CAF na kusonga...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

USIKU wa deni haukawii, hatimaye ile siku iliyokuwa inasubiriwa na mashabiki wa soka Tanzania kuona timu zao zinatinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa imefika.

Si wengine, ni Simba, Yanga, Azam FC na Kipanga zinatarajia kushika dimbani kwa muda na nchi tofauti kwa ajili ya mechi za marudiano za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Jijini Dar es Salaam, Simba watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Primeiro de Agosto kutoka Angola, mechi itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni, wenyeji Simba wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi ugenini wa mabao 3-1, mechi iliyofanyika kwenye Uwanja wa 11 Novembro, Luanda.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi ya mchezo wa leo yamekamilika kwa asilimia 90.

Mgunda alisema wachezaji wote wa timu hiyo wako kwenye hali nzuri huku wakiwa na ari na utayari kuipigania klabu kwa kuwapa furaha mashabiki wao pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Kocha huyo alisema wanakutana na timu ambayo wameiona na wanawajua ubora wao, hivyo wamejiandaa kuhakikisha wanatumia vizuri mapungufu yao kupata ushindi nyumbani.

"Naweza kusema maandalizi yamekamilika kwa asilimi 90, wachezaji wote wapo katika hali nzuri kuhakikisha wanatetea bendera ya taifa na kuwapa furaha Wanasimba," alisema Mgunda.

Aliongeza katika mchezo wa leo ataendelea kukosa huduma ya beki wao wa kulia, Shomari Kapombe ambaye anaendelea kupona majeraha yake na Jimmyson Mwanuke.

Wakati huo huo, Yanga watashuka ugenini jijini Khartoum, Sudan kuanzia saa 3:00 usiku kwa saa za Tanzania kuwakabili wenyeji Al Hilal, katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga iliyoondoka alfajiri ya kuamkia juzi itakuwa na kazi moja tu ya kusaka ushindi ili kutinga hatua ya makundi, ambapo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1998 ilipofanya hivyo kwa mara ya mwisho.

Kwenye mechi ya kwanza nchini Jumamosi iliyopita, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1, hivyo kwenye mechi ya leo hata kama haikupata ushindi, ili ifuzu inatakiwa walau itoke sare ya zaidi ya bao moja.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia gazeti hili akili yake na ya wachezaji iko katika mechi hiyo ambayo wanakwenda kusaka matokeo chanya kwa ajili ya mashabiki wao.

"Tumecheza mechi ya kwanza, sasa tunakwenda kucheza mechi ya pili, kila mchezaji akili yake iko kwenye mechi hii. Tunajua ni ngumu kucheza mbele ya umati ule ya mashabiki wa Al Hilal, lakini tuna wachezaji wenye uzoefu wa kucheza kwenye hali kama ile kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Tanzania, kama Al Hilal walipata bao Dar es Salaam, basi na sisi tunaweza kupata tukiwa ugenini, najua ni timu nzuri na hata msimu uliopita waki-

INAENDELEA UK. 23

## Serengeti Girls yaichapa Ufaransa

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), imeweka historia ya kupata ushindi baada ya kuifunga Ufaransa mabao 2-1 katika mechi ya Kundi D katika Fainali za Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Pandt Jawaharial Nehru, Goa nchini India.

Kwa ushindi huo, Serengeti Girls imepanda hadi katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa kundi hilo linaloongozwa na Japan na kufufua matumaini ya kusonga mbele endapo itafanya vizuri kwenye mechi ya mwisho.

Katika mechi ya kwanza ya mashindano hayo, Serengeti Girls ilikubali kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa mabingwa watetezi, Japan.

Mchezaji Diana Mnaly, aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza wa soka nchini na wa wanawake kufunga bao katika michuano hiyo kwa kuipatia Tanzania bao dakika ya 17.

Diana aliukwamisha wavuni mpira kwa mguu wa kulia, akiunganisha kona iliyopigwa na Aisha Mnuka, wachezaji wote wa Simba Queens.

Serengeti Girls ingekwenda mapumziko ikiwa na mabao mawili kama si Koku Kipanga kupaisha juu penalti dakika ya 39 iliyotokana na Mnuka aliyekuwa anaenda kufunga kukanyagwa na beki mmoja wa Ufaransa katika eneo la hatari.

Dakika 15 baada ya kipindi cha pili Serengeti Girls ilipata bao la pili lililofungwa kwa penalti baada ya beki wa Ufaransa, Elimbi Gilbert, kuunawa mpira katika harakati za kuokoa hatari langoni mwake.

Alikuwa ni Christer Buhera, aliyeukwamisha wavuni na kumwacha kipa wa Ufaransa, Feerine Belhardj, akiruka bila mafanikio.

Bao hilo lilionekana kuwazindua Wafaransa ambao walianza kulishambulia lango la Tanzania kama nyuki, lakini mabeki wa timu hiyo wakiongozwa na kipa, Zulfa Makau, walikaa imara kuzuia hatari zote.

Ufaransa ilifanikiwa kupata bao la kufutia machozi dakika ya 77 likifungwa kwa penalti na mchezaji wao machachari, Lucia Calba.

Sekunde chache kabla mechi kumalizika, Joyce Lema wa Serengeti Girls alionyeshwa kadi nyekundu ikiwa ni ya pili kwenye mechi hiyo ya pili.

Serengeti Girls itashuka tena dimbani keshokutwa kucheza mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kwa kuivaa Canada wakati Japan wao watavaana na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >